

**ATHARI ZA KIISIMU ZA LAHAJA YA KIMAKUNDUCHI
KATIKAKISWAHILI SANIFU KINACHOTUMIKA SHULENI
MAKUNDUCHI ZANZIBAR**

SALEH ABDELSALAM MOHAMMED SALEH

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA
MASHARTI YA DIGIRII YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI YA CHUO
KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2013

UTHIBITISHO

Aliyetia saina hapa chini anathibitisha kuwa amesoma Tasinifu hii iitwayo: '*Athari za Kiisimu za Lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu Kinachotumika Shuleni Makunduchi Zanzibar*', na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digirii ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Prof. Y.M. Kihore

(Msimamizi 1)

Tarehe

Dkt. P.P.Lipembe

.....
(Msimamizi 2)

.....
Tarehe

IKIRARI

NA

HAKI MILIKI

Mimi, SALEH ABDELSALAM MOHAMMED SALEH, natamka na kuthibitisha kwamba tasnifu hii, iitwayo *'Athari za Kiisimu za Lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu Kinachotumika Shuleni Makunduchi Zanzibar'* ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba haijawahi kuhudhurishwa popote kwa lengo la kufuzu shahada yoyote.

Sahihi

Tarehe

Haki ya kunakili Tasinifu hii inalindwa na mkataba wa Berne, Sheria ya haki ya kunakili ya mwaka 1999 na mikataba mingine ya sheria za kitaifa na kimataifa zinazolinda mali ya kitaaluma. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama yote au sehemu ya Tasinifu hii, isipokuwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa wazazi wangu na familia yangu baada ya kuwa mbali nayo
kwa muda mrefu.

SHUKRANI

Kwa hakika binadamu aliye muungwana haachi kutoa shukrani zake kwa lolote lile alipatalo. Nimefunzwa kwamba wa awali anayestahiki kushukuriwa ni Mola Muumba wa ulimwengu huu na vilivyomo ndani yake. Namshukuru sana kwa kunipa uzima wa siha, nguvu za mwili, na wasaa wa kushiriki kwenye kozi hii tokea mwanzo hadi mwisho. Laiti kama si mapenzi yake kwangu, ningeshindwa kufikia hatua hiyo. Pili, nawashukuru wazazi wangu kwa kunilea, kunihurumia, kunifunza na kunifundisha kwa kila lililo jema.

Tatu, nalishukuru taifa langu kwa kunidhamini masomo haya tokea mwanzo hadi hatima. Ni faraja ilioje kwangu na kwa familia yangu dhidi ya msaada huo. Nne, naushukuru uongozi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kunijali, kunithamini, pamoja na kuniadini hadi kufikia hatua ya kunisajili kuwa miongoni mwa wanafunzi wa kozi hii. Nasema shukrani sana. Tano, namshukuru msimamizi wangu wa kazi hii Prof. Kihore. Kwa hakika nimejifunza mengi kutoka kwake. Amenisaidia na kushirikiana nami katika kila hali. Nakiri kuwa Prof. Kihore, atabaki kuwa kumbukumbu ya milele isiyosahaulika.

Mwisho, nawashukuru watu wote walioshirikiana nami katika kuifanikisha kazi hii. Wapo wengi na wala siwezi kuwataja wote, nitawabainisha wachache tu. Miongoni mwao ni Omar Salum Mohamed wa SUZA aliyekuwa msaidizi wangu, Mw. Juma Ali Simai wa Makunduchi, Mw. Jabir Alzarouq na Moli Alzarouq, wote wa Qatroun Libya, Bw. Said Khamis Said (dereva wa tekisi) wa Kinondoni Mkwajuni Dar es Salaam na wengineo. Shukrani za pekee zimwendee Sheikh, Prof. Sengo kwa kunijali na kunielekeza katika mambo mbalimbali.

IKISIRI

Utafiti huu uliwalenga wanafunzi wa skuli za msingi na sekondari za Makunduchi zilizo katika wilaya ya Kusini Unguja katika kuchunguza athari za Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu. Pia, walimu wa somo la Kiswahili walishirikishwa kikamilifu. Kwa upande wa wanafunzi, waliotafitiwa ni watoto wenye umri kati ya miaka 10-14 ambao ni wanafunzi wa msingi; na miaka 15 – 20 wanaosoma sekondari. Mbinu kadhaa zilitumika ikiwemo mbinu ya usaili, mbinu ya kutumia hojaji, mbinu ya maktaba, mbinu ya uchunguzi wa maskanini na mbinu ya majaribio. Kila mbinu ilimsaidia mtafiti kwa namna moja au nyingine wakati wa ukusanyaji wa data; na pia wakati wa uchambuzi.

Utafiti huu una sura tano. Sura ya kwanza imefafanua usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, umuhimu, upeo wake na pia imebainisha kiunzi cha nadharia kilichotumiwa na utafiti huu. Sura ya pili imeelezea mapitio ya maandiko ambapo mna mjadala wa namna fulani kuhusiana maandiko hayo na namna yalivyomsaidia mtafiti katika kazi yake. Sura ya tatu imezungumzia mbinu alizotumia mwandishi katika ukusanyaji wa data yake. Sura ya nne imewasilisha uchambuzi wa data. Katika uwasilishaji huo, sura imeanza kwa kubainisha sifa za kiisimu za lahaja ya Kimakunduchi kwa ujumla, pia imebainisha matumizi ya Kimakunduchi madarasani pamoja na kuonesha athari za lahaja hiyo kwa Kiswahili Sanifu. Sura ya tano imeonesha matokeo ya utafiti ambapo imebainika kwamba yamekidhi haja ya maswali ya utafiti yaliyotumika kama dira ya ukusanyaji wa data. Mwisho, sura ya sita imemaliza kwa kuonesha muhtasari na mapendekezo ya utafiti.

YALIYOMO

UTHIBITISHO	i
IKIRARI NA HAKI MILIKI	ii
TABARUKU.....	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI	v
YALIYOMO.....	vi
ORODHA YA MAJEDWALI	x
SURA YA KWANZA	1
1.0 UTANGULIZI WA JUMLA.....	1
1.1 Usuli wa Tatizo	1
1.2 Tatizo la Utafiti	4
1.3 Malengo ya Utafiti	4
1.3.1 Lengo Kuu	4
1.3.2 Malengo Mahususi.....	5
1.4 Maswali ya Utafiti.....	5
1.5 Umuhimu wa Utafiti	5
1.6 Upeo wa Utafiti.....	7
1.7 Mipaka ya Utafiti	7
1.8 Vikwazo vya Utafiti.....	7
1.9 Utatuzi wa Vikwazo vya Utafiti.....	8
1.10 Kiunzi cha Nadharia.....	8
1.11 Hitimisho.....	10

SURA YA PILI.....	11
2.0 MAPITIO YA MAANDIKO.....	11
2.1 Utangulizi.....	11
2.2 Maandishi Yenyewe.....	11
2.3 Hitimisho.....	14
SURA YA TATU.....	16
3.0 MBINU ZA UTAFITI.....	16
3.1 Utangulizi.....	16
3.2 Eneo la Utafiti	16
3.3 Uteuzi wa Sampuli	16
3.4 Mbinu za Kukusanyia data.....	17
3.4.1 Data za Upili	17
3.4.2 Data za Msingi	18
3.4.2.1 Utafutaji wa Mtafiti Msaidizi.....	18
3.4.2.2 Mbinu ya Usaili.....	18
3.4.2.3 Mbinu ya Hojaji	19
3.4.2.4 Mbinu ya Maktaba	20
3.4.2.5 Mbinu ya Uchunguzi wa Maskanini	20
3.4.2.6 Mbinu ya Majaribio	21
3.5 Zana za Utafiti.....	21
3.6 Uchambuzi wa Data	21
3.7 Hitimisho.....	22
SURA YA NNE	23
4.0 UCHAMBUZI WA DATA	23
4.1 Utangulizi.....	23

4.2	Sifa za Kiisimu za Kimakunduchi	23
4.3	Sauti za Kimakunduchi	23
4.3.1	Maumbo ya Maneno ya Kimakunduchi.....	28
4.3.1.1	Maneno ya Kimakunduchi na Ujitoshelezaji wa Kimaana	28
4.3.1.2	Maneno ya Kimakunduchi na Viambishi vya Nafsi	29
4.3.1.2.1	Maumbo ya Maneno na Njeo.....	31
4.3.1.3	Maumbo ya Maneno ya Umilikishi	32
4.3.1.4	Maumbo ya Maneno ya Udondoshaji	33
4.3.1.5	Maumbo ya Maneno na Utofauti wa Msamiati	34
4.3.1.6	Maumbo ya Maneno na Ukanushi	35
4.3.1.7	Maumbo ya Maneno na Mnyambuliko.....	36
4.3.1.8	Maumbo ya Nomino za Kimakunduchi	39
4.3.2	Tungo za Kimakunduchi	41
4.3.2.1	Tungo Katika Hali ya Kiima na Kiarifu.....	41
4.3.2.2	Tungo za Kimakunduchi na Upatanishi wa Kisarufi	42
4.4	Matumizi ya Kimakunduchi Madarasani	43
4.4.1	Matumizi ya Lugha darasani.....	43
4.4.1.1	Lugha ya Wanafunzi	45
4.4.1.2	Lugha ya Walimu.....	47
4.4.2	Matini za Walimu	49
4.4.2.1	Lugha ya Muhtasari wa Masomo.....	50
4.4.2.2	Kazi za Wanafunzi	52
4.5	Athari za Kimakunduchi kwa Kiswahili.....	57
4.5.1	Athari za Kiisimu	57

4.5.1.1	Athari katika Sauti	58
4.5.1.1	Athari katika Maneno	60
4.5.1.2	Athari katika Tungo	64
4.5.1.2.1	Tungo Kirai	65
4.5.1.2.2	Tungo Kishazi	67
4.5.1.2.3	Tungo Sentensi.....	68
4.5.2	Athari kwa Utoaji Elimu	71
4.5.2.1	Athari kwa Masomo Yanayofundishwa.....	73
4.5.2.2	Athari katika Ujifunzaji	75
4.5.2.3	Athari katika Ufundishaji.....	77
4.5.3	Taathira ya Athari Hizo.....	78
4.6	Hitimisho.....	84
SURA YA TANO		86
5.0	MATOKEO YA UTAFITI.....	86
5.1	Utangulizi.....	86
5.2	Matokeo	86
5.2.1	Matokeo Kutokana na Maswali ya Utafiti	86
5.2.2	Taathira za Dhana za Kinadharia	90
SURA YA SITA.....		94
6.0	MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	94
6.1	Utangulizi.....	94
6.2	Muhtasari na Hitimisho la Utafiti	94
6.3	Mapendekezo ya utafiti.....	96
MAREJELEO		98

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na.1: Konsonanti Katika Kimakunduchi	24
Jedwali Na. 2: Sauti za Kimakunduchi zenye Ukonsonanti.....	26
Jedwali Na. 3: Sauti za Kimakunduchi zenye Uvokali	27
Jedwali Na. 4: Eneo ambalo Sauti zenye Uvokali hutolewa.....	27
Jedwali Na 5: Viwakilishi Nafsi Viambata katika Vitenzi.....	30
Jedwali Na. 6: Njeo za Kimakunduchi	31
Jedwali Na. 7: Hali ya Umilikishi	32
Jedwali Na. 8: Udondoshaji katika Lahaja ya Kimakunduchi	33
Jedwali Na 9: Kuhusu Maumbo ya Maneno na Utofauti wa Kimsamiati.....	34
Jedwali Na.10: Hali ya Uyakinishi na Ukanushi katika Kimakunduchi	35
Jedwali Na.11: Maumbo ya Maneno na Mnyambuliko.....	36
Jedwali Na. 12: Kiima na Kiarifu Katika Lahaja ya Kimakunduchi	42

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Usuli wa Tatizo

Maelezo kuhusu lahaja za Kiswahili yalianza kujitokeza siku nyingi. Miongoni mwa kazi za mwanzo ni ile ya Stigand (1915). Katika kazi yake, Stigand anaeleza kuwa lengo lake lilikuwa ni kusambaza, kadri iwezekanavyo, maneno mengi ya lahaja kutokana na hofu kwamba mabadiliko makubwa yaliyokuwa yakitokea yangeweza kusababisha kupotea kwake. Hivyo, kimsingi kazi yake ilijihusisha zaidi na orodha ya maneno ya lahaja kwa nia ya kuyahifadhi kimaandishi. Vilevile, Stigand (ameshatajwa) amebainisha lahaja 15 za Kiswahili ambazo kwa wakati huo bado ubainishi wake haukufanyika kwa misingi ya kitaaluma.

Mbaabu (1991), kwa upande wake, anaelezea changamoto zilizokuwepo mwishoni mwa karne ya 19 katika harakati za kuichagua lahaja moja ya kuisanifisha. Pamoja na changamoto zilizokuwepo, mwishowe, lahaja ya Kiunguja Mjini ikasanifiwa. Jambo hilo likasababisha kuibuka kwa lahaja ya Kiswahili Sanifu iliyopewa hadhi ya kutumika katika sehemu za kazi, kwenye vyombo vya kutunga sheria, na maandishi yake kutawala kwenye vitabu kadhaa vya kitaaluma. Kamati na mabaraza mbalimbali yakaundwa kwa lengo la kukitetea Kiswahili Sanifu (Maganga, 1997).

Kamati na mabaraza hayo yalifanya kazi yake na hatimaye kukubaliana kwamba lahaja ya Kiunguja Mjini ndiyo isanifishwe na kuwa Kiswahili Sanifu. Hata hivyo, ni jambo lisilopingika kwamba, wengi kati ya wanakamati hao walikuwa ni wazungu ambao hakuwa na ujuzi wa kutosha katika taaluma ya lugha hususani lugha ya

Kiswahili na lahaja zake. Kutokana na ukweli huu kulikuwa na makosa mengi katika usanifishaji wa lugha ya Kiswahili uliofanywa na watu hao (Maganga, 1997). Pamoja na makosa hayo kuwepo Kiswahili Sanifu kilichofanywa na watu hao ndicho kilichokubalika na serikali na kutumika katika shughuli rasmi kama vile elimu, utawala, mahakama na katika mikutano ya hadhara.

Mbaaabu (2003) anaeleza kwamba, lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi kiasi kwamba zile zinazofahamika kwa wataalamu wa lugha ya Kiswahili ni chache tu kutokana na kutozitifiti vya kutosha. Anaendelea kueleza kwamba, jambo lililowafanya wataalamu hao wa Kiswahili kutoitafiti lugha hii kwa upana unaostahiki ni dhana kwamba Kiswahili Sanifu ndiyo hasa Kiswahili chenyewe na hivyo kupuuzi lahaja mbalimbali za Kiswahili. Anasema kwamba, athari za lahaja mbalimbali za lugha ya Kiswahili katika Kiswahili Sanifu zinaonekana bayana katika namna mbalimbali lakini utashangaa kuona kwamba wataalamu hao hawazioni jambo linalofanya wasizimakinikie kiutafiti kama inavyopasa. Maelezo haya yametupatia changamoto na chachu ya kufanya utafiti wa kina ili kuona lahaja ya Kimakunduchi in athari gani katika Kiswahili Sanifu.

Masebo na Nyangwine (2006; 2007; 2008) katika ufafanuzi wao juu ya maana ya lahaja katika lugha ya Kiswahili pamoja na mambo mengine wanakiri kwamba kuna tofauti mbalimbali zinazojitokeza kutoka lahaja moja na nyingi. Miongoni mwa mambo yanayotofautisha lahaja hizo ni lafudhi, fonolojia na msamiati. Maelezo haya yanatoa ufahamu kwamba kama kuna tofauti za kifononolojia, msamiati na lafudhi kati ya lahaja moja na nyingine ni dhahiri kwamba kuathiriana kwa lahaja hizo katika vipengele hivyo ni jambo lisilopingika. Tunasema hivi kwa sababu jamii ya

Wamakunduchi kwa mfano, huzungumza Kimakunduchi katika shughuli na mawasiliano mbalimbali katika sehemu kubwa ya maisha yao ya kila siku. Kwa msingi huu, wanapokuwa katika shughuli rasmi ambapo wanalazimika kuzungumza Kiswahili Sanifu ni wazi kwamba athari za Kimakunduchi zitajitokeza katika Kiswahili Sanifu bila hata ya wao kutarajia. Msanjila (2006) anaeleza kwamba ni vigumu sana kuitenganisha jamii na lugha yake kwa kuwa lugha na jamii ni kama pande mbili za sarafu moja.

Kitala (2006) anaeleza kwamba, utamaduni uliopo ndani ya lugha ya Kiswahili hubainika katika lahaja zake. Anaendelea kueleza kwamba ukitaka kuufahamu vizuri utamaduni wa lugha ya Kiswahili basi pitia lahaja zake mbalimbali ndipo utaona utajiri wa utamaduni upatikanao katika lugha ya Kiswahili. Suala kwamba katika lugha kumesheheni utamaduni wa jamii husika ni jambo lisilopingika kwa namna yoyote ile kwa kuwa ni jambo la kweli ambalo limethibitishwa na tafiti mbalimbali ambazo zimeshafanyika. Maelezo haya yanakazia uelewa wetu kwamba kama katika lugha ndimo mna utamaduni wa jamii husika basi ni vigumu utamaduni huu kujificha pale mzungumzaji wa lugha hiyo anapozungumza lugha ama lahaja nyingine tofauti na ile ya kwake. Kimakunduchi kina utamaduni wake kama zilivyo lugha ama lahaja nyingine za lugha ya Kiswahili jambo ambalo linafanya mzungumzaji wa Kimakunduchi kudhihirisha utamaduni huo pale anapozungumza Kiswahili Sanifu. Katika kudhihirisha utamaduni huo ndipo athari za Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu huonekana.

Hivyo basi, wanafunzi na walimu wao wanapokuwa shuleni husisitizwa kutumia Kiswahili Sanifu katika mawasiliano mbalimbali baina yao. Hata hivyo, pamoja na

msisitizo huo bado hujitokeza athari mbali mbali zikiwemo za kiisimu za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu kitumikacho shuleni. Kwa msingi huo basi, utafiti huu umefanywa ili kubainisha athari za kiisimu za lahaja ya Kimakunduchi zinazojitokeza katika Kiswahili Sanifu katika shule teule za Makunduchi Zanzibar.

1.2 Tatizo la Utafiti

Kutokana na kukua na kupanuka kwa matumizi ya Kiswahili Sanifu katika mazingira rasmi, kumekuwa na mijadala mingi kuhusu athari ya lugha hii kwa lugha nyingine za kijamii (taz. k.m. Mochiwa, 1979; Rubanza, 1979). Lakini imewahi pia kuchunguzwa jinsi lugha hizi za kijamii zinavyoathiri matumizi ya Kiswahili hasa katika mazungumzo pale matamshi ya lugha ya kijamii yanapojitokeza katika Kiswahili. Hata hivyo, mijadala kama hii haijawahi kuhusisha lahaja za Kiswahili ambazo nazo ni lugha za kijamii na zenye uhusiano na lahaja sanifu na vile vile uwezekano wa kuathiri lahaja hiyo sanifu.

Kwa kuwa mtafiti hakubahatika kuona kazi iliyochunguza athari za lahaja mbalimbali katika mazingira yaliyo rasmi; utafiti huu ulichunguza athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu katika maeneo rasmi ya sekta ya elimu.

1.3 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yalikuwa kama hivi ifuatavyo:

1.3.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ilikuwa kuchuguzwa athari za lahaja ya Kimakunduchi katika msamiati wa Kiswahili hususani katika maeneo rasmi ya kielimu.

1.3.2 Malengo Mahususi

- i. Kubainisha sifa za kiisimu za lahaja ya Kimakunduchi.
- ii. Kufafanua athari za kiisimu zilizopo baina ya lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu.
- iii. Kueleza taathira za athari hizo kwenye matumizi ya Kiswahili Sanifu katika maeneo rasmi ya sekta ya elimu.

1.4 Maswali ya Utafiti

- i. Je ni zipi sifa za kiisimu za lahaja ya Kimakunduchi?
- ii. Lahaja ya Kimakunduchi ina athari gani katika msamiati wa Kiswahili Sanifu?
- iii. Je ni zipi taathira za athari hizo katika matumizi ya Kiswahili Sanifu katika maeneo ya elimu?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Leo hii, Kiswahili kimepiga hatua kubwa katika kukua na kuenea kwake. Nchini Tanzania lugha ya Kiswahili imeenea kila mahali na watu wengi hukizungumza na kukijadili. Taifa limekuwa moja, na takribani watu wote wanaelewana kwa kutumia lugha hii. Kiswahili ni lugha ya Taifa katika nchi za Tanzania, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hivi sasa lugha hii ipo katika mchakato wa kuwa lugha ya mawasiliano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na mojawapo miongoni mwa lugha rasmi za Umoja wa Afrika (AU).

Lahaja Sanifu huwa lengo lake ni kufanikisha mawasiliano ya namna moja katika masuala yote rasmi kama vile utoaji wa elimu, utekelezaji wa sheria, n.k. Hivyo,

haitarajiwi lahaja sanifu kukabiliwa na athari zinazovuruga lengo hili. Hii ndiyo inafanya tuchunguze athari za lahaja ya Kimakunduchi kwenye lugha rasmi ili kubaini zilivyo na faida au hasara zake kiisimu kwa eneo husika. Utafiti kama huu unaweza kuchochea tafiti katika maeneo mengine ili kubaini vipengele vya athari hizi vinavyoweza kuwa kikwazo kwa mawasiliano kupitia lugha rasmi.

Kinadharia utafiti huu ni muhimu katika kuthibitisha baadhi ya nadharia za kiisimu jamii hasa zile zinazoeleza kwamba wanaadamu hawazungumzi lugha moja ama ileile katika mazingira yale yale. Katika mazingira ya shule wanafunzi pamoja na walimu wao husisitizwa wazungumze lugha ya Kiswahili Sanifu jambo ambalo haliwezekani kwa mujibu wa nadharia tulizodokeza. Tunasema haliwezekani kwa sababu lugha mama ya kila mzungumzaji lazima itamuathiri mzungumzaji katika mawasiliano yake kupitia lugha rasmi. Hali hii inathibitisha nadharia za isimu jamii kwamba ni vigumu kumtenga mwanadamu na lugha yake.

Kitaaluma: utafiti huu utakuwa rejeleo muhimu ambalo litatumiwa na wahadhiri pamoja na wanafunzi wao wa shahada za awali, umahiri na uzamivu. Kwa upande wa wahadhiri utafiti huu utawawezesha kuandaa mihadhara yao juu ya masuala ya lahaja na kuwafundisha wanafunzi wao masualan haya kwa ufasaha wake. Kwa upande wa wanafunzi watautumia utafiti huu kama sehemu ya mapitio yao ya kazi tangulizi ili kukamilisha tafiti zao.

Usanifishaji wa lugha: utafiti huu utasaidia kuonesha athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu jambo ambalo linaweza kuongeza msamiati mpya katika Kiswahili sanifu. Baadhi ya misamiati ya lahaja ya Kimakunduchi

ambayo inatumika sambamba na Kiswahili sanifu inaweza kusanifiwa na kuwa sehemu ya lugha rasmi.

1.6 Upeo wa Utafiti

Katika kuzitafiti athari za Kimakunduchi dhidi ya lahaja sanifu katika shule mbali mbali za Makunduchi, mtafiti alijihusisha na kipengele cha ufundishaji na tathmini kwa wanafunzi.

Kwa upande wa ufundishaji athari hizi ziliangaliwa kwa walimu kupitia katika matini yao ya kufundishia na namna wanafunzi wanavyoshiriki katika majadiliano.

Kwa upande wa utahini tulichunguza namna mitihani inavyoandaliwa na majibu ya wanafunzi. Mitihani hii ilijumuisha mazoezi mbalimbali ya darasani na mitihani ya katikati na mwishoni wa muhula.

1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kuchanguza athari za kiisimu za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu. Katika utafiti huu hatutajikita katika kuchunguza athari nyingine za lahaja hii katika Kiswahili Sanifu. Tumeamua kufanya hivi ili kuweza kukamilisha malengo yetu ya utafiti kwa muda uliopangwa.

1.8 Vikwazo vya Utafiti

Kikwazo kikubwa katika utafiti huu kilikuwa ni ugeni wa mtafiti katika mazingira ya Tanzania kwa kuwa yeye binafsi ni mzaliwa wa Libya. Mtafiti huyu ni mgini wa utamaduni wa Watanzania jambo ambalo ilikuwa kikwazo kwake kuingiliana na kuchanganyika nao katika utafiti wao. Vile vile, mtafiti si mahiri sana katika

kuzungumza lugha ya Kiswahili jambo ambalo pia lilimzuia kuwasiliana kwa urahisi na watafitiwa wake.

1.9 Utatuzi wa Vikwazo vya Utafiti

Vikwazo vya utafiti tulivyovianisha hapo juu vilitatuliwa kwa mtafiti kutafuta mtafiti msaidizi ambaye ni mahiri katika lugha ya Kiswahili na anauelewa wa kutosha wa utamaduni na mazingira ambayo mtafiti aliyateua kwa ajili ya utafiti wake ambayo ni maeneo ya Makunduchi Zanzibar. Msaidizi huyu wa utafiti amefanya kazi nzuri ya kumwelekeza mtafiti mambo yote ambayo mtafiti alihitaji msaada.

1.10 Kiunzi cha Nadharia

Kazi ya utafiti ilihitaji kuongozwa na nadharia yenye kukubaliana na mada husika. Mtafiti alitumia ‘Nadharia ya Umaumbo’ iliyoasisiwa na mhakiki maarufu wa Urusi, Michail Mikhailovich Bakhtin katika mwaka 1917.

Bakhtin katika nadharia hii, amejihusisha zaidi na dhana iliyowashughulisha wasomi na wanataaluma wengi juu ya mseto wa vilugha mbalimbali-muundo changamano wa vijilugha, yaani, lahaja za lugha husika. Vijilugha hivyo hutofautisha vipengele kadhaa kama makundi, umri, na vizazi. Kwa mujibu wa mhakiki huyu, kila kimoja ya vipengele hivyo, kina thamani na hujaribu kuelezea tajriba kadhaa. Anaendeleza mawazo yake kwa kusema kwamba, vilugha hivi vina kawaida ya kushindana katika kila kauli. Anaamini kuwa kila tamko lina athari au ‘maburuzo’ ya matamko mengine yanayolitangulia au yatakalolifuatia kama majibu

au uitikio. Kwake yeye, lugha ni mivutano kati ya mifumo mbalimbali katika jamii (Wamitila. 2002).

Maelezo hayo yanasisitiza mambo makuu yafuatayo ambayo yalikuwa muhimu katika utafiti huu. Mosi, lugha ya Kiswahili ni mseto wa lahaja mbalimbali. Hivyo, muundo huo kupitia lahaja zake umekiathiri Kiswahili Sanifu. Utafiti huu ulizichunguza athari hizo.

Pili, lugha katika jamii hutofautisha makundi, umri na vizazi. Yaani, matumizi ya lugha, iwe ya kimazungumzo au kimaandishi, humtambulisha anayeisikia au kuisoma, kuelewa ni akina nani wanaoongea (makundi), rika lao likoje (umri), na hata jinsia. Jambo hili nalo ni muhimu. Sifa hiyo ilimuongoza mtafiti kwa kuufanya utafiti huu kulingana na makundi mbalimbali. Makundi aliyoyateuwa yalikuwa ya walimu, wanafunzi na maafisa wa elimu.

Tatu, nadharia imebainisha kuwa lugha ni mivutano ya mifumo mbalimbali. Ni dhahiri kuwa madamu kuna athari ya tamko kati ya lugha moja na nyingine, suala la mivutano ni la kawaida. Hivyo, mtafiti pia alichunguza ni mivutano ipi iliopo ya lahaja sanifu na lahaja ya Kimakunduchi.

Kwa ujumla, nadharia hii ndio iliyotumiwa na mtafiti katika utafiti huu hasa kwa vile alibaini kuwa inaendana na mwelekeo wa malengo ya utafiti huu kama yalivyoorodheshwa hapo awali.

1.11 Hitimisho

Sura hii ni ya utangulizi wa utafiti mzima ambapo vipengele mbalimbali vya kiutangulizi vimewasilishwa. Miongoni mwa vipengele hivyo ni pa,oja na usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo nya utafiti na utatuzi wake na kiunzi cha nadharia. Vipengele vyote hivi kwa pamoja vimetusaidia katika kupata uhalali wa kufanyika kwa utafiti wetu. Tunayasema haya kwa sababu ni kutokana na vipengele hivi ndimo tatizo la utafiti lilipobainishwa. Sura inayofuata inafanya upitiaji wa maandiko na machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti wetu.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA MAANDIKO

2.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ameweka mapitio kadhaa aliyoyapitia kabla ya kuihalalisha mada yake kwa kigezo cha kuchunguza iwapo imewahi kutafitiwa au la. Mapitio yote aliyoyasoma hayakudhihirisha kufanyika utafiti huo. Alichobaini kwamba wapo watafiti walioitafiti lahaja ya Kimakunduchi, pia wapo waandishi walioiandikia ingawa si katika mwelekeo kama wa utafiti huu.

2.2 Maandishi Yenyewe

Whiteley (1956) alifanya utafiti kuhusu lahaja ya Ki-mtang'ata. Katika kazi yake ameelezea zaidi juu ya matamshi ya lahaja hiyo. Jambo muhimu aliloligusia ni kwamba lahaja zina sifa zake zenye kutofautiana baina ya lahaja moja na nyingine. Pamoja na hayo, yapo baadhi ya mambo yaliyo mahususi katika kila lahaja, kama vile mashina ya maneno. Kazi hii ilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa vile iliweza kumsaidia mtafiti kupata mwelekeo wa kuzielewa sifa za lahaja ambazo zilimwongoza katika kuzielewa sifa za kiisimu za lahaja iliyotafitiwa na hivyo kuwa rahisi katika kuainisha athari za lahaja tafitiwa katika Kiswahili sanifu.

Mohamed (1984) alifanya utafiti unaohusiana na lahaja za Kipemba, Kiunguja mjini pamoja na Kiswahili Sanifu. Utafiti wake ulijihusisha zaidi na kuelezea matamshi ya lahaja ya Kipemba, pamoja na kuzungumzia jinsi ukanushi unavyojitokeza ndani ya lugha hizo. Katika uchambuzi wake, amedhihirisha mambo mawili makubwa. Kwanza, misamiati kadhaa ya lahaja ya Kipemba na jinsi inavyotofautiana na Kiswahili Sanifu, na pia ameonsha mabadiliko ya sauti mbali mbali na jinsi

zinavyotofautiana kutoka maeneo ya mjini hadi vijijini. Aidha, ameonesha umilikishaji wa lahaja ya Kipemba ambao kwa kiasi kikubwa hutokea ndani ya nomino husika kama: nyumbayo' badala ya nyumba yako, 'pahalape' badala ya pahala pake, na 'kisungwa' badala ya kisu cha watu. Ni dhahiri kuwa vipengele hivyo vya lahaja ya Kipemba vilimsaidia mtafiti kupata mwongozo wa mambo ya kuyafanyia kazi wakati wa utafiti wake hususani wakati wa kuzichunguza sifa za kiisimu za lahaja ya Kimakunduchi.

Maganga (1991) katika tasnifu yake ya Uzamivu amezitungumzia lahaja tatu za Zanzibar. Lahaja hizo ni Kipemba, Kimakunduchi na Kitumbatu na kuzihusianisha na Kiswahili sanifu. Dhamira kuu ya kazi yake ni kuchunguza mofofonolojia ya lahaja za Kipemba, Kitumbatu, na Kimakunduchi huku akizihusianisha na Kiswahili Sanifu. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti huu. Kazi hii ilimsaidia mtafiti kupata baadhi ya misamiati ya Kimakunduchi, na pia kupata mwongozo wa uchambuzi wa data zake. Maganga (1997) aliongelea pia suala la lahaja. Alizitaja lahaja mbali mbali za kusini na kaskazini, na kueleza jinsi lahaja zinavyotofautiana kati yao. Katika kielelezo cha lahaja mama ya kusini, amekionyesha Kimakunduchi na hivyo, kumwezesha mtafiti kuelewa asili ya lahaja aliyoifanyia utafiti.

Masebo na Nyangwine (2008) wameendeleza kuzitungumzia lahaja za Kiswahili. Wamesema kuwa 'Lahaja ni mojawapo ya lugha ambazo kusema kweli huhesabika kama lugha moja isipokuwa zinatofautiana katika baadhi ya vipengele kama vile lafudhi, fonolojia (matamshi), msamiati usiokuwa msingi au miundo'. Aidha, wameziorodhesha aina mbali mbali za lahaja na kuanisha eneo inamopatikana kila lahaja. Hata hivyo, kazi hii haikukidhi haja ilivyokusudiwa na utafiti huu kutokana

na sababu zifuatazo. Kwanza, kazi ya akina Masebo na Nyangwine (wameshatajwa) haikujihusisha na lahaja mahsusi kama utafiti huu ulivyofanya. Pili, utafiti huu ulichunguza athari za Kimakunduchi kwa lahaja sanifu, ilhali kazi ya akina Masebo imezungumzia lahaja kwa ujumla wake.

Mbaabu (1991) aliandika kitabu kinachohusu historia ya Kiswahili na usanifishaji wake. Katika kuielezea historia hiyo anaeleza kuwa ingawa kulikuwa na lahaja nyingi, lakini lahaja za Kimvita na Kiunguja ndizo zilizokuwa katika ushindani mkubwa katika mchakato wa kuteua lahaja moja ambayo ndiyo itakuwa msingi wa Kiswahili Sanifu. Hata hivyo pamoja na ushindani uliokuwepo hatimae lahaja ya Kiunguja ikateuliwa kuwa msingi wa Kiswahili Sanifu. Kazi ya Mbaabu ilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa kuwa ilimsaidia mtafiti kufahamu historia ya lugha ya Kiswahili na lahaja zake ambayo iliweza kutoa nuru kwa utafiti husika.

Kitala (2006) katika makala yake ya amezungumzia juu ya ripoti ya Semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA) iliyowasilishwa na Katibu Mtendaji wa Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA). Katika ripoti hiyo imeelezwa kuwa nafasi nyingine ya utamaduni ndani ya lugha ya Kiswahili imo kwenye lahaja za lugha hiyo. Zimetajwa baadhi ya lahaja kama vile Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi kuwa zimehifadhi utajiri mkubwa wa msamiati unaoafikiana na shughuli za kila siku za jamii husika. Mfano mzuri ni Kamusi ya Kitumbatu yenye misamiati mingi ihusuyo uvuvi na mazao ya baharini. Ripoti hii ni uthibitisho kwamba Kimakunduchi ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili, kama ilivyodhihirika katika kazi ya Masebo na Nyangwine (2007), Mhilu na Masebo (2008), na Khamis (2008).

Mwansoko, (2008) katika makala yake ameelezea juu ya umuhimu wa kuzidi kuzifanyia utafiti lahaja za Kiswahili. Amesema kuwa katika kukiendeleza na kukiimarisha Kiswahili Sanifu ni budi watafiti wazidi kuzitafiti lahaja ili ziweze kujaza mapengo ya misamiati na kiistilahi. Maelezo ya makala hii yalitusukuma na kututia hamu ya kufanya utafiti wa kina katika kuchunguza athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu.

Massamba na wenzake (2009) wameelezea historia fupi ya Kiswahili pamoja na kuonyesha lahaja za Kiswahili. Katika maelezo yao wamesema kuwa, yapo mambo ya kimsingi yenye kutofaitisha lahaja moja na nyingine. Miongoni mwa mambo hayo ni matamshi, msamiati, muundo na wakati mwingine maana ya maneno. Maelezo haya yanafanana na yale ya Muhura (2009) ambaye ameorodhesha jumla ya lahaja 18 za Kiswahili na amesema kuwa miongoni mwa mambo yenye kupelekea lugha moja kuwa na lahaja tofauti ni umbali wa kijiografia, hamahama ya watu, elimu na uhaba wa mawasiliano kati ya jamii moja na nyingine. Kazi hizo zilikuwa muhimu. Zilimwongoza mtafiti kuzielewa baadhi ya sifa zinazoweza kuitofautisha lahaja moja na nyingine.

2.3 Hitimisho

Sura hii imefanya mapitio ya kazi tangulizi ambazo zinahusiana na mada ya utafiti huu kwa lengo la kutaka kufahamu nini hasa kimeshatafitiwa kuhusiana na masuala ya lahaja kwa ujumla na pia lahaja ya Kimakunduchi kimahususi. Katika mapitio haya tumegundua kwamba watafiti watangulizi wamefanya kazi kiasi katika kutafiti lahaja za Kiswahili kwa ujumla wake. Hata hivyo kazi waliyoifanya bado ni ndogo sana ikilinganishwa na masuala ya lahaja za Kiswahili ambayo yanahitaji kutafitiwa.

Kwa mfano, hatujafanikiwa kukutana na kazi tangulizi inayohusiana na athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu. Kutokana na ukweli huu ndio maana tukaamua kufanya utafiti wa kina katika kuchunguza athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu. Sura inayofuata inafanya uwasilishaji wa mbinu mbalimbali za ukusanyaji na uchambuzi wa data.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sehemu hii imezungumzia mbinu kadhaa ambazo mtafiti alizitumia katika kuitekeleza kazi yake. Aidha, sehemu hii imeweka bayana mfuatano wa matukio, kubainisha eneo la utafiti, kundi lengwa la utafiti, uteuzi wa sampuli, jinsi data zilivyo kusanywa, vifaa vilivyotumika wakati wa kazi yenyewe, na mwisho, jinsi uchambuzi wa data ulivyo fanyika.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika kisiwani Unguja katika Wilaya ya Kusini, eneo la Makunduchi. Uteuzi wa eneo hili ulifanyikakutokana na sababu zifuatazo. Mosi, wakaazi wengi wasema Kimakunduchi wanaishi huko na ndiko kwenye shule zilizotafitiwa.

Pili, Wamakunduchi wanasifika sana katika kuitumia lahaja yao popote pale walipo. Hivyo, mtafiti alitaka kuthibitisha iwapo matumizi hayo ya lahaja hutumika pia shuleni na hivyo kuathiri hata somo la Kiswahili ambalo kwa kawaida hutumia lahaja sanifu.

3.3 Uteuzi wa Sampuli

Mtafiti ameteua sampuli ambayo ilikuwa ni kiwakilishi cha kujibu maswali yaliyolengwa katika utafiti huu. Sampuli iliteuliwa kwa kutumia kigezo cha umri, viwango vya elimu na jinsia. Rika lililotafitiwa lilijumuisha watoto wenye umri kati

ya miaka 10 – 14 ambalo kwa kawaida huwa ni rika la watoto wa shule za msingi, na rika kati ya miaka 15 – 20 ambalo ni rika kwa wanafunzi wa sekondari.

3.4 Mbinu za Kukusanyia data

Kukusanya data ni zoezi la awali katika utafiti. Kothari (1990) anasisitiza kuwa hatua ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji data. Katika utafiti huu mtafiti alikusanya data za msingi na upili. Data za upili zilikusanywa kwa kutumia mbinu za maktabani huku data za msingi zikikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili, hojaji, upitiaji wa nyaraka, uchunguzi wa maskanini na majaribio.

3.4.1 Data za Upili

Data za upili ni aina ya data katika utafiti wowote ule wa kitaaluma ambazo hukusanywa kutoka katika maandiko na machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti (Kothari, 2008). Madhumuni hasa ya kukusanya data hizi ni kujaziliza data za msingi ili kusaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Data hizi hukusanywa kutoka katika vitabu, makala, majarida, tasnifu, magazeti, tovuti na wavuti. Ili kuweza kuzipata data hizi mtafiti alilazimika kwenda maktaba mbalimbali kutafuta maandiko yanayohusiana na mada yake na utafiti na kuyasoma kwa kina. Miongoni mwa maktaba alizozitembelea ni pamoja na Maktaba kuu ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Maktaba ya Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Maktaba na Makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Maktaba ya Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar na Maktaba Kuu ya Taifa.

3.4.2 Data za Msingi

Data za msingi kwa kawaida huwa ni data ghafi ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti kwa ajili ya kujibu maswali yake ya utafiti na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine yeyote kwa minajili ya utafiti kama huu unaokusudiwa kufanywa hivi sasa (Kothari, 2008). Data hizi hukusanywa masikanini kutoka kwa watafitiwa mbambali walioteuliwa na mtafiti na ambao anatambua kwamba watampatia data muafaka zitakazosaidia kujibu maswali yake ya utafiti. Data hizi pia hukusanywa kwa kutumia mbinu mbalimbali ambazo tumezianisha hapa chini. Kabla ya kuziainisha mbinu hizo tueleze kwanza kipengele cha utafutaji wa mtafiti msaidizi

3.4.2.1 Utafutaji wa Mtafiti Msaidizi

Mtafiti ni mzaliwa wa Libya aliyekuja Tanzania kwa nia ya kujifunza lugha ya Kiswahili. Hivyo, ni mgeni wa mazingira na kwa utamaduni wa watu aliokwenda kuwatafiti. Aidha, ni mchache wa ufasaha wa lugha yao. Hivyo, alilazimika kuwa na mtafiti msaidizi aliyeweza kumsaidia kwa kumpeleka katika eneo lake la utafiti. Pia, alimsaidia kwa kutoa ufafanuzi uliyo fasaha wakati wa mahojiano yake na watafitiwa. Aidha, msaidizi pia alimsaidia katika kumrekebishia na kumsahihishia maneno, na miundo ya sentensi wakati wa uandishi wa ripoti hii.

3.4.2.2 Mbinu ya Usaili

Mbinu hii inahusisha uwasilishaji wa maswali kwa wasailiwa. Maswali hayo yalijibiwa kwa njia ya mdomo na kurikodiwa katika kinasa sauti, na pia kuandikwa kwenye daftari la kumbukumbu. Kwa mujibu wa Kothari (1990) mbinu hii inaruhusu utoaji wa ufafanuzi pale inapoonekana taarifa fulani haijaleweka vema

wakati wa kuuliza maswali. Mbinu hii hatimaye husaidia kuweka bayana istilahi ambazo zinaonekana hazieleweki kwa watu wanaoulizwa maswali. Pia inasaidia kupata taarifa za ziada na za kina zaidi; hususani pale ambapo majibu ya watu wanaosailiwa yanapokuwa hayaeleweki. Vile vile, usaili ulimsaidia mtafiti kugundua mahusiano magumu katika mahusiano ya kijamii na hivyo kumuwezesha kuwa karibu na watoa habari.

Hivyo basi, katika utafiti huu usaili ulitumika ili kupata data zilizohusiana na taathira za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu. Kadhalika, kupitia mbinu hii mtafiti aliwauliza watafitiwa wake maswali ya aina moja na yaliyo katika mpangilio uliyo sawa. Mtafiti aliandaa maswali yaliyolenga kukusanya taarifa za aina moja kwa kila kundi la watafitiwa ambao ni wazungumzaji wa Kimakunduchi, walimu na wanafunzi katika shule zilizoteuliwa.

3.4.2.3 Mbinu ya Hojaji

Hojaji kwa mujibu wa Kothari (1990) ni mbinu ya utafiti ambapo mtafiti anaandaa maswali yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani. Maswali haya yanaweza kuhitaji majibu mafupi au marefu kutegemeana na taarifa inayohitajika na mtu anayepewa hojaji hizo. Mbinu hutoa fursa kwa mtafiti kuwaachia watafitiwa hojaji ili wajaze kwa muda wao halafu huzikusanya baada ya muda waliokubaliana kufika. Fursa hii inamfanya mtafiti kupata muda wa kuendelea na shughuli zake nyingine wakati watafitiwa wakiwa wamebaki na hojaji hizo wakizijaza. Hata hivyo, wakati mwingine, baadhi ya watafitiwa huwa hawarejeshi hojaji au huzirejesha pasipo kuzijaza jambo ambalo huwa ni hasara kwa mtafiti. Hata hivyo udhaifu huu hutatuliwa pale mtafiti anapokuwa ametumia mbinu zaidi ya moja katika ukusanyaji

wake wa data. Data ambazo hazikupatikana kupitia hojaji zitapatikana kupitia mbinu nyingine. Katika utafiti huu mbinu hii ilitumiwa zaidi kwa walimu walioteuliwa.

3.4.2.4 Mbinu ya Maktaba

Mbinu inahusisha mapitio ya kazi mbalimbali zilizofanywa na watafiti waliotangulia zenye kuhusiana na kazi hii. Kazi hizo zinaweza kuhusu nadharia mbalimbali au hata uchambuzi wa dhana zinazohusiana na mada ya utafiti husika kwa namna moja ama nyingine (Kothari, 1990). Katika utafiti huu mtafiti alikwenda katika maktaba alizozitaja hapo juu ili kupitia na kusoma maandishi mbalimbali yenye kuhusiana na mada yake. Lengo lilikuwa ni kuchunguza wataalamu wengine wanasema nini kuhusiana na mada ya utafiti na pia kupata data za kujazilizia data za msingi. Pia, katika kupitia maandishi hayo mbalimbali katika maktaba kulimsaidia mtafiti kujifunza mengi yaliyomo kwenye kazi za wenzake pamoja na kuzidi kuangalia nadharia na mbinu kadhaa zilizohusiana na utafiti huu.

3.4.2.5 Mbinu ya Uchunguzi wa Maskanini

Mtafiti kwa kusaidiana na msaidizi wake walifika maskanini na kuchunguza mawasiliano ya kiufundishaji na ya kimazungumzo ya wanafunzi na walimu kwa lengo la kupata data sahihi juu ya athari za lahaja hiyo katika Kiswahili Sanifu. Mtafiti na msaidizi wake waliingia darasani ili kuona namna wanafunzi na walimu wanavyowasiliana kwa lengo la kupata data sahihi kwa mujibu wa utafiti huu. Vile vile, mtafiti na msaidizi wake walitoka nje ya madarasa wakati wa mapumziko ya wanafunzi na kuchunguza mawasiliano yao wawapo nje ya darasa kwa lengo lilelile la kupata data sahihi.

3.4.2.6 Mbinu ya Majaribio

Katika mbinu hii mtafiti alitunga maswali kadhaa na kuwafanyia majaribio wanafunzi wa skuli teule za Makunduchi ili kuona iwapo maandishi yao yameathiriwa na lahaja yao ya Kimakunduchi. Majaribio hayo yalizingatia zaidi ujibuji wa maswali kutokana na habari waliyopewa, pamoja na kutoa insha za maelezo marefu ambazo ziliweza kutuonesha athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu.

3.5 Zana za Utafiti

Utafiti ulitumia zana kama vile kinasa sauti, daftari na kalamu, pamoja na hojaji. Kinasa sauti kilimsaidia mtafiti katika kunasa sauti za watafitiwa wake kwa kumbu kumbu ya baadaye wakati wa uchambuzi wa data.

Kwa upande wa daftari na kalamu, vifaa hivi vilitumika kwa kuandika baadhi ya taarifa muhimu zilizotolewa na watafitiwa. Taarifa hizo ziliandikwa kwa muhtasari, lakini wenye kueleweka. Muhtasari huo ndiyo uliomwezesha mtafiti kujua ni vipi aanze uchambuzi wa data zake, na hatimaye, kuandika ripoti ya kazi nzima. Pia mtafiti aliandaa hojaji zenye maswali kadhaa na kuwapatia watafitiwa ambao walizijaza na kutupatia data zilizowezesha kuandikwa kwa tasinifu hii.

3.6 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kipengele muhimu katika kukamilisha utafiti uliokusudiwa kufanywa kwa namna iliyokusudiwa. Babbie (1999) anaeleza kwamba, uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data data zilizokusanywa kwa namna ambayo inawezesha kukamilisha malengo ya utafiti husika. Kothari (2008)

anaeleza kwamba uchambuzi wa data ni hatua muhimu katika utafiti ambayo husaidia kutafuta majibu ya tatizo la utafiti. Hivyo basi, katika utafiti huu mbinu za uchambuzi wa data za kimaelezo na kimaheسابu ndiyo ziliyotumika katika uchambuzi wa data kama inavyoonekana katika sura ya nne ya utafiti wetu. Mbinu ya uchambuzi wa data ya kimaelezo inaelezwa kama mbinu isiyohusisha mahesabu bali ni maelezo ya kina tu ndiyo hutolewa katika kufafanua data ili kukamilisha malengo ya utafiti (Kothari). Mbinu ya uchambuzi wa kimaheسابu ni ile inayohusisha tarakimu kama vile asilimia na idadi ya watafitiwa ama vitafitiwa. Mbinu zote hizi mbili zimetumika katika uchambuzi wa data za utafiti wetu. Vile vile, katika uchambuzi wa data za utafiti wetu tumetumia majedwali ambamo ndani yake mna data za utafiti ambazo zimechambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo. Mbinu hii ya uchambuzi wa data imekuwa muafaka katika utafiti huu kwa sababu inaendana na aina ya utafiti wetu.

3.7 Hitimisho

Sura hii imefanya uwasilishaji wa mbinu mbalimbali ambazo zimetumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu kama zinavyojitokeza katika sura ya nne ya tasinifu hii. Mbinu za ukusanyaji wa data za uwandani na maktabani ndizo zilizotumiwa katika ukusanyaji wa data za utafiti huu. Uchanganyaji wa mbinu za utafiti za maktabani na uwandani umetoa fursa ya kukusanya data ambazo ni muafaka tena zilizosaidia kujibu maswali yetu ya utafiti. Kwa upande wa mbinu za ukusanyaji wa data uwandani tumetumia mbinu zaidi ya moja jambo ambalo limesaidia kutatua udhaifu wa mbinu moja kutokana na ubora wa mbinu nyingine na hivyo kutupatia data muafaka. Sura inayofuata inafanya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti.

SURA YA NNE

4.0 UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Kabla ya uchambuzi wa data kuuona ni vyema tuzungumzie sifa za kiisimu za Kimakunduchi katika ujumla wake. Hili ni jambo muhimu ambalo linasaidia kuzielewa vyema athari zilizobainika kwenye utafiti huu. Baadaye tuchunguze matumizi ya lahaja hiyo yanavyojitokeza madarasani. Mwisho, tuweze kuziona athari za lahaja hiyo kwa Kiswahili Sanifu.

4.2 Sifa za Kiisimu za Kimakunduchi

Lahaja ya Kimakunduchi ni asasi mojawapo muhimu ambayo hadi sasa bado haijaathiriwa sana na lahaja jirani au na lugha nyingine. Kimakunduchi hutumika sana Kusini mwa kisiwa cha Unguja, Zanzibar (Chum, 1994). Naye Maganga (1991) anasema kuwa Kimakunduchi husikika sana kusini na mashariki ya Zanzibar. Lahaja hii ndiyo inayotambulikana kama lahaja ya Kimakunduchi. Chum (ameshatajwa) anakiri kuwa lahaja hii ina maneno mengi yenye asili ya Kiswahili, ilhali machache sana ni yenye asili za kigeni. Katika sura hii mtafiti ameelezea vipengele vitatu muhimu. Navyo ni, sauti, maumbo ya maneno, na tungo za Kimakunduchi.

4.3 Sauti za Kimakunduchi

Awali, tumegusia kwamba lahaja hii inazo sauti ambazo ndizo zinazoungana na kuunda maneno. Maganga (1991) anaeleza kuwa lahaja hii ina jumla ya irabu tano, na konsonanti 25, kuashiria kwamba sauti za Kimakunduchi ni 30. Katika kuzichunguza sauti hizo, utafiti umebaini kuwa hakuna tofauti ya sauti zilizomo katika lahaja hiyo na lahaja sanifu ya Kiswahili. Katika kulithibitisha hili, umetumika

utaratibu wa kutumia mifano ya jozi bainifu inayotokana na lahaja yenyewe ya Kimakunduchi. Tuzingatie jedwali lifuatalo:

Jedwali Na.1: Konsonanti Katika Kimakunduchi

Mfano wa Jozi Bainifu	Sauti Iliyopatikana	Maana ya Maneno ya Jozi Bainifu
beta/peta	/b/, /p/	Beta – 1. <i>kumba mkono</i> 2. <i>tengenea</i> Peta - 1. <i>kufa. Mfano</i>
baja/bata	/t/, /ʃ/	Baja – 1. <i>toka maji</i> Bata – 1. <i>jifunga, anza</i>
bedua/bekua	/d/, /k/	Bedua – 1. <i>tenganisha</i> Bekua – 1. <i>kukaidi kwa ghafla</i> 2. <i>kutenganisha kwa kupeta</i>
Buga/bunda	/g/, /nd/	Buga - 1. <i>tikisika, hangaika</i> Bunda – 1. <i>Bahasha</i>
bwesa/bweka	/s/	Bwesa – 1. <i>chana</i> Bweka – 1. <i>chanika. pasuka</i>
chacha/chaka	/tʃ/	Chacha – 1. <i>kazana</i> 2. <i>nyauka</i> Chaka – 1. <i>taka, hitaji</i> 2. <i>haraka, upesi</i>
chaki/chali	/l/	Chaki – 1. <i>majimoto (aina ya mdudu)</i> Chali – 1. <i>jando</i> 2. <i>kumbi</i>

chana/chata	/n/	Chana – 1. <i>mchana</i> Chata – 1. <i>Furahia</i>
chewa/cheza	/w/, /z/	Chewa – 1. <i>chelewa</i> Cheza – 1. <i>Chenza</i>
yenga/denga	/y/	Yenga – 1. <i>tembea, kwenda huko na huko</i> 2. <i>tunza</i> Denga – 1. <i>Tuama</i>
dhambi/kwambi	/ð/	Dhambi – 1. Kwambi – 1. <i>shuka ya marekani</i>
Shaki/chaki	/ʃ/	Shaki – 1. <i>kasirika, hamaki</i> Chaki – 1. <i>majimoto (aina ya mdudu)</i>
ng'aza/taza	/ŋ/	Ng'aza – 1. <i>tambua, elewa, fahamu</i> Taza – 1. <i>popoa</i>
nyama/zama	/ɲ/	Nyama – 1. <i>mnyama</i> Zama – 1. <i>jifiche</i>
fuza/vuza	/f/, /v/	Fuza – 1. <i>funza</i> Vuza – 1. <i>Lainisha</i>
kwera/kweta	/r/	Kwera – 1. <i>shuwari, hali ya kutulia, kuwa kimya</i> Kweta – 1. <i>Sota</i>
aka/ama	/m/	Aka – 1. <i>pita msimokuwa na njia, rukiarukia</i> Ama – 1. <i>kama, iwapo. Ikiwa</i>

Baada ya kuziona sauti hizo, sasa tuangalie jedwali lifuatalo ambalo linatuonesha mahali ambapo sauti hizo hutokea na jinsi zinavyotamkwa.


Jedwali Na. 2 : Sauti za Kimakunduchi zenye Ukonsonanti

JINSI YA KUTAMKA	MAHALI PA KUTAMKIA							
		Midomo	Midomo	Ufizi	Ufizi	Kaakaa	Kaakaa	Koromeo
			Meno	Meno		Gumu	Laini	
VIPASUO	Ghuna	B			D		g	
	Viso ghun	P			T		k	
VIZUIA KWAMIZI	Ghuna					J		
	Viso ghun					tʃ		
VIKWAMIZI	Ghuna		v	ð	Z			h
	Viso ghun		F	θ	S	f		
NAZALI		M			N	ɲ	ŋ	
VITAMBAZA					L			
VIMADENDE					R			
VIYEYUSHO		W				Y		

Jedwali Na. 3: Sauti za Kimakunduchi zenye Uvokali

Mfano wa Jozi Bainifu	Sauti Inayopatikana	Maana ya maneno ya Jozi Bainifu katika Kiswahili Sanifu
Botoa/botea	/o/, /é/	Botoa – 1. <i>vunja kama dafu</i> Botea – 1. <i>mmea unaoota zaidi ya mwaka mmoja</i>
Chau/chao	/u/	Chau – 1. <i>pwani</i> Chao – 1. <i>hali ya kutaga</i>
Kitu/kutu	/i/	Kitu – 1. <i>paka mweusi, paka mwitu</i> Kutu – 1. <i>choo, kinyesi, mavi</i>
Kola/kolo	/a/	Kola – 1. <i>chuma</i> Kolo – 1. <i>tamani, mwenye tama</i>

Sasa tuangalie jedwali linalofuata ili tuone eneo la ulimi ambalo sauti zenye uvokali hutolewa.

Jedwali Na. 4 : Eneo ambalo Sauti zenye Uvokali hutolewa

Kwa ujumla, tunaona kwamba jedwali Na. 2 na Na. 4 yamebainisha sauti za lahaja ya Kimakunduchi. Katika jedwali Na. 2 tunaona mambo mawili makubwa. Moja, mahali ambapo sauti hizo zenye ukonsonanti hutokea; na jinsi zinavyotamkwa. Jedwali linatuonesha kuwa, sauti hizo hutamkwa kwenye midomo, kwenye midomo na meno, kwenye ufizi na meno, kwenye ufizi, kwenye kaakaa gumu, kwenye kaakaa laini, na pia katika koromeo.

Kwa upande wa vokali, tunaona kuwa jedwali Na.4 linabainisha maeneo mbali mbali ya utokeaji wa sauti hizo. Yaani, kuna sauti inayotolewa mbele ya ulimi katika eneo lake la juu /i/, nyengine hutokea huko huko juu nyuma ya ulimi /u/, sauti nyingine hutolewa sehemu ya kati ya ulimi, na nyengine ni sauti /a/ inayotolewa chini ya ulimi.

4.3.1 Maumbo ya Maneno ya Kimakunduchi.

Katika kipengele hiki, tumejaribu kuelezea maumbo ya maneno ya Kimakunduchi. Maumbo hayo yamechunguzwa katika hali zifuatazo. Kwamba je, yanajitosheleza kimaana, je yanachukuwa viambishi vya aina tofauti kama vile viambishi vya nafsi, wakati, urejeshi, n.k, na je, yanakubali mnyambuliko wa maneno?

4.3.1.1 Maneno ya Kimakunduchi na Ujitoshelezaji wa Kimaana.

Kwa mujibu wa Chum (1994), Kimakunduchi kinajitosheleza na ndiyo maana kinatumika katika mawasilisano ya Wamakunduchi. Anasema, ‘... Kwa kawaida Wamakunduchi wanapokutana kuongea faragha hutumia lafudhi yao, yaani, Kikae, wakati wanapongea na wengineo hutumia lugha sanifu’. Kauli hiyo ni muhimu na inayostahiki kuthaminiwa. Lugha yenye kutumika katika maongezi ya kila siku, ni

dhahiri kuwa si pungufu. Hata hivyo, inahofiwa lugha hii kupotea siku hadi siku kwa sababu haina matumizi mapana. Chum (1994) anaendelea kusema kuwa, *'Kamusi ya lahaja ya Kikae imetengenezwa kwa madhumuni maalumu... pamoja na maingiliano ya jamii nyinginezo utakuta kuwa ndimi za vizazi vilivyotangulia zinahitilafiana sana na ndimi za vizazi vya siku hizi, sembuse hivyo vijavyo...'* (uk.1-2). Utamkaji wa maneno ya Kimakunduchi unalazimu uzawa, uasili na ukaazi wa Makunduchi. Haiyumkiniki, asiye mzaliwa kuitamka lugha hii katika upeo wa ufanisi wake. Haya yamethibitishwa na Rais wa Nne wa Zanzibar Almarhoum Idris Abdul Wakili katika dibaji yake ya *Kamusi ya msamiati wa Pekee wa Kikae* (1994). Anasema, *'... ni shida sana kwa mtu ambaye hakuzaliwa na hasa kukulia Makunduchi kuweza kukisema kwa fasaha nzuri. Watu wengi hujaribu kukisema lakini mara nyingi hushindwa katika matamshi. Kwa sababu hiyo baadahi ya watu hufikiri kuwa Kikae ni lugha tofauti na Kiswahili.*

4.3.1.2 Maneno ya Kimakunduchi na Viambishi vya Nafsi

Unafsi ni moja ya sifa zenye kujenga maumbo ya maneno ya Kiswahili, na aghalabu hutokea katika vitenzi. Neno unafsi lina maana ya matumizi ya nafsi katika vitenzi vya Kimakunduchi. Katika kulichunguza hili, mtafiti amebaini kuwa vitenzi vya lahaja ya Kimakunduchi vinayo sifa ya kubeba nafsi katika hali zote. Yaani, hali ya umoja na wingi, na pia, katika hali ya utenda na utendwa. Tuchunguze jedwali lifuatalo:

Jadwali Na 5: Viwakilishi Nafsi Viambata katika Vitenzi

	KIAMBISHI NAFSI	MFANO KATIKA UTENDA	KIAMBISHI NAFSI	MFANO KATIKA UTENDA
NAFSI YA KWANZA	ni-	niwamo	ni-	Anione - aḡonE
UMOJA WINGI	tu-	tuwavano	tu-	atuone – atone
NAFSI YA PILI	ku-	kuwamo	ku-	akuuze – akuze
UMOJA WINGI	wa-	wawavano	wa-	
NAFSI YA TATU	ka-	kawavano	mu-	
UMOJA WINGI	wa-	Wawavano	wa-	

Jedwali Na. 5 linaonyesha matumizi ya nafsi katika hali ya umoja na wingi katika muktadha wa utenda na utendwa. Hii inadhihirisha kuwa vitenzi vya lahaja ya Kimakunduchi vinabeba sifa ya unafsi kama ilivyo kwenye Kiswahili Sanifu. Hata hivyo, kwa kuwa Kimakunduchi ni lahaja, zipo tofauti chache zinazojitokeza kati ya nafsi za lahaja sanifu na lahaja ya Kimakunduchi. Lahaja Sanifu kwa mfano, nafsi

yake ya pili wingi, na ya tatu umoja, huwakilishwa kwa kiambishi nafsi kiambata ‘u-’ na ‘a-’, ilhali kwa upande wa lahaja ya Kimakunduchi huwakilishwa kwa ‘ku-’ na ‘ka’ kwa upande wa utenda. Pia, kwa upande wa utendwa, nafsi ya tatu (umoja) ya lahaja sanifu huwakilishwa na kiambishi ‘m-’, ilihali, katika lahaja ya Kimakunduchi huwakilishwa na ‘mu-’.

4.3.1.2.1 Maumbo ya Maneno na Njeo

Njeo ni asasi muhimu katika mjengeko wa maneno. Huweka bayana utofauti wa wakati ambao tendo hutokea. Yaani, njeo hufahamisha wakati tendo lilipotokea, linapotekea au litakapotekea. Waandhisi wengi wa sarufi ya Kiswahili wamezibainisha njeo katika namna tatu. Yaani, kuna njeo ya wakati tulionao yenye kuwakilishwa na mofimu ‘-na-’, njeo ya wakati ujao inayowakilishwa kwa ‘-ta-’, na jeo ya wakati uliopita ambayo huwakilishwa kwa ‘-me-’ iwapo wakati uliopita ni muda mfupi, na kwa ‘-li-’ iwapo umepita wakati mrefu. Lahaja ya Kimakunduchi inazo njeo hizo hizo. Hebu tuangalie jedwali lifuatalo kwa uzingatifu.

Jadwali Na. 6: Njeo za Kimakunduchi

Aina ya Njeo	Kiambishi cha Njeo	Mfano katika uyakinishi	Mfano katika ukanushi
Wakati uliopita	-li-	Niliona	Sijaona
Wakati uliopita	-me-	Kumekwimba	Sitjakwimba
Wakati tulionao	-na-	Kunakwangasa	Sinakwangasa
Wakati ujao	- tʃʌ (ta)	Tuaimtʃʌimba	Hatʃʌuchakwimba

Jedwali Na. 6 hapo juu linabainisha njeo zilizomo katika lahaja ya Kimakunduchi. Ni dhahiri kuwa njeo zilizomo katika jedwali hilo hazitofautiani na njeo za lahaja sanifu. Isipokuwa, katika Kiswahili sanifu, kiambaishi cha njeo yake ni ‘-na-’ ilihali katika lahaja ya Kimakunduchi huwakilishwa na kiambishi ‘-cha-’. Vivyo hivyo, katika ukanushi, hakuna mabadiliko ya njeo kati ya lahaja sanifu na lahaja ya Kimakunduchi.

4.3.1.3 Maumbo ya Maneno ya Umilikishi

Lahaja ya Kimakunduchi inayo sifa ya kubeba dhana ya umilikishi ndani ya maumbo ya maneno yake. Yaani, kwa baadhi ya wakati, umbo la neno; na hasa nomino, huweza kubeba kiambishi cha umilikishi na hivyo kulifanya neno hilo lionyeshe umilikishi ndani yake. Tuangalie viambishi vya umilikishi katika jedwali lifuatalo.

Jedwali Na. 7: Hali ya Umilikishi

Nafsi	Shina la umilikishi	Mfano
Kwanza	-angu (umoja)	Mtoto wangu
	-etu (wingi)	Mtoto wetu
Pili	-ako (umoja)	Mtoto wako
	-enu (wingi)	Mtoto wenu
Tatu	-ake (umoja)	Mtoto wake
	-ao (wingi)	Mtoto wao

Katika lahaja ya Kimakunduchi, umilikishi katika maumbo ya maneno hujitokeza kwa kuunganishwa neno na baadhi ya silabi zenye kuonyesha umilikishi. Kwa

mfano, katika nafsi ya tatu (umoja), ‘*mtoto wake*’ huunganishwa kwa pamoja na kuwa ‘*mtotowe*, ‘*rafiki yake*’ kuwa ‘*rafikiye*’ na ‘*rafiki yako*’ kuwa ‘*rafikiyo*’.

4.3.1.4 Maumbo ya Maneno ya Udondoshaji

Katika lahaja ya Kimakunduchi, udondoshaji unajitokeza katika aina nyingi za maneno. Tuchunguze jadwali lifuatalo, na kisha tuweze kupata ufafanuzi wa yale yaliomo ndani ya jedwali hilo.

Jedwali Na. 8: Udondoshaji katika Lahaja ya Kimakunduchi

Mfano wa Udondoshaji katika Nomino	Mfano Katika Vivumishi/Viwakilishi	Mfano katika Vitenzi	Mfano katika Vielezi	Mfano katika Vihusishi/Viunganishi
Chi- Nchi Mfano: Chi inabaja (<i>Nchi inatoka maji</i>)	yo-huyo mfano: Afikiyo yo? (<i>Ni rafiki yako huyo?</i>)	Nda- nakwenda Mfano: Nda vangusa mabui (<i>Nakwenda kupangusa mabuibui</i>)	chi-chini Mfano: Ukangua situpe chi. (<i>Ukichuma usitupe chini</i>)	n’kuku – nakuku Mfano: Asije kwakulwa n’kukuyo (<i>Asije akapapurwa na kuku huyo</i>)

Jedwali Na. 8 hapo juu linabainisha namna udondoshaji unavyojitokeza katika nomino, vivumishi/viwakilishi, vitenzi, vielezi na vihusishi/viunganishi. Jambo hili linadhahirisha utajiri wa kuitumia lugha ya Kimakunduchi katika udondoshaji wa

maneno. Tumbaine kuwa, katika nomino kuna baadhi ya viambishi vinaweza kudondoshwa kama ‘*nchi*’,- ‘*chi*’, na hivyo hivyo, katika vivumishi/viwakilishi ‘*yo*’ –‘*huyo*’, kwenye vitenzi ‘*nda*’ – ‘*nakwenda*’, kwenye vielezi ‘*chi*’ – ‘*chini*’ na kwenye vihusishi ‘*n’kuku*’ – ‘*na kuku*’.

4.3.1.5 Maumbo ya Maneno na Utofauti wa Msamiati

Licha ya kutambulika kuwa Kimakunduchi ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili, kuna utofauti mkubwa wa kimsamiati kati ya lahaja hiyo na lahaja sanifu. Katika dibaji ya Msamiati wa Pekee wa Kikae ilioandikwa na Rais wa Nne wa Zanzibar, Mhe. Idris Abdul Wakil anasema: ‘...kwa sababu hiyo baadhi ya watu hufikiri kuwa Kikae ni lugha tofauti na Kiswahili.’ Bila ya shaka, maneno hayo yalivyoelezwa, ndivyo ilivyo. Kukifahamu Kimakunduchi kwa mtu asiye Mmakunduchi, ni shida mno. Hii inatokana na utofautia mkubwa uliopo kati ya msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi na lahaja sanifu ya Kiswahili. Hebu tuangalie mifano michache katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na 9: Kuhusu Maumbo ya Maneno na Utofauti wa Kimsamiati

	Kimakunduchi	Kiswahili Sanifu
i	Kiya – Kiya akakwa huyagisa	<i>Kila – Kila apewapo huipoteza</i>
ii	Njo- Uyoko njo mwachagisa	<i>Ndiyo/ye – Yule ndiye aliyekipoteza</i>
iii	Nga- usivyo mwavwa hauvata chembe	<i>Hata – usipomsaidia hataupata</i> <i>hata chembe nga</i>
iv	Ja-Cho! Ja ayo hayachacha/kwa	<i>Kwa-He! Kwa haya hayatatakiwa</i>

Jedwali Na. 9 hapo juu linabainisha utofauti wa kimsamiati unaojitokeza baina ya lahaja ya Kimakunduchi na lahaja sanifu. Mtafiti ametumia maneno manne (*kila*, *ndiye*, *hata*, *kwa*) kama mifano hususiya, yenye konyesha utofauti wa lahaja mbili hizo. Neno '*kila*' katika Kiswahili Sanifu hutamkika 'kiya' katika lahaja ya Kimakunduchi. Vile vile, neno '*ndiye*' linakuwa 'njo', 'hata' linabadilika na kuwa 'nga', na neno '*kwa*' linakuwa 'ja'. Hata hivyo, tunaporejelea sentensi zote nne zilizomo ndani ya jedwali hilo, tunabaini kuwa maneno mengi yaliyotumika katika sentesi za lahaja sanifu ya Kiswahili yamebadilika na kuwa mengine kabisa wakati yalipotumika katika lahaja ya Kimakunduchi. Mathalan, neno '*kupewa*' katika Kiswahili Sanifu ni 'kukakwa' katika Kimakunduchi, au '*kupoteza*' ni 'kugisa', '*kusaidia*' ni 'kumwavwa', '*kupata*' ni 'kuvata', '*he!*' ni 'cho!', na '*kutakiwa*', ni 'kuchakwa'. Kwa hivyo, kupitia sentesi hizo tunaweza kuunga mkono kauli ya Mhe. Idris Abdul Wakil kwamba, mgeni wa Kimakunduchi anaweza kudhani kuwa lahaja hiyo si Kiswahili. Haki ya kudai hivyo ipo. Maana idadi kubwa ya maneno yanayotumika katika lahaja hiyo hayamo katika Kiswahili Sanifu.

4.3.1.6 Maumbo ya Maneno na Ukanushi

Kimakunduchi ni lugha yenye kubeba ukanushi 'ndani' na 'nje' ya maneno yake. Ipo mifano mingi yenye kuthbitisha kauli hii. Tuchunguze jedwali hili:

Jedwali Na. 10: Hali ya Uyakinishi na Ukanushi katika Kimakunduchi

	Hali ya Uyakinishi	Hali ya Ukanushi
i.	<i>tupa</i> – ukangua tupa chi	<i>situpe</i> – ukangua situpe chi
ii.	<i>Anguwa</i> – angua kwa ngowiko	<i>usanguwe</i> - usanguwe kwa ngowiko
iii.	<i>njo</i> -uyoko njo mwakwaza	<i>so</i> – uyoko so mwakwaza

Jedwali Na. 10 hapo juu linaonyesha hali ya uyakinishi na ukanushi unaojitokeza katika lahaja ya Kimakunduchi. Mfano wa kwanza na wa pili unaonyesha namna ukanushi unavyojitokeza ndani ya umbo moja la neno, ilhali mfano wa tatu unabainisha jinsi ukanushi unavyojitokeza ndani ya maneno mawili.

4.3.1.7 Maumbo ya Maneno na Mnyambuliko

Licha ya hali tofauti za maumbo ya maneno ya Kimakunduchi, utafiti ulibaini kuwa maneno ya lahaja hii yanayo sifa ya kukubali mnyambuliko mithili ya maneno ya lahaja sanifu. Tuchunguze mifano ifuatayo:

Jedwali Na.11: Maumbo ya Maneno na Mnyambuliko

Neno Kuvika-Kupika	Kauli ya:	Mnyambuliko wake
	Kutenda	Vika
	Kutendea	Vikia
	Kutendeka	Vikika
	Kutendewa	Vikiwa
	Kutendeana	Vikianani
	Kutendwa	Vikwa
	Kutendesha	Vikisha
Kuwapa-Kutafuta	Kutenda	Wapa
	Kutendea	Wapia
	Kutendeka	Wapika

	Kutendewa	Wapiwa
	Kutendeanana	Wapianani
	Kutendwa	Wapwa
	Kutendesha	Wapisha
Kuvwaza-Kuchemsha	Kutenda	Vwaza
	Kutendea	Vwazia
	Kutendeka	Vwazika
	Kutendewa	Vwaziwa
	Kutendeanana	Vwaziwanani
	Kutendwa	Vwazwa
	Kutendesha	Vwazisha
Kugwia-Kukamata	Kutenda	Gwia
	Kutendea	Gwilia
	Kutendeka	Gwilika
	Kutendewa	Gwiliwa
	Kutendeanana	Gwilianani
	Kutendwa	Gwiwa
	Kutendesha	Gwilisha
Kuvita-Kupita	Kutenda	Vita
	Kutendea	Vitia

	Kutendeka	Vitika
	Kutendewa	Vitiwa
	Kutendeanana	Vitianani
	Kutendwa	Vitwa
	Kutendesha	Vitisha
Kuchowea-Kusema	Kutenda	Chowea
	Kutendea	Chowezea
	Kutendeka	Chowezeka
	Kutendewa	Chowezewa
	Kutendeanana	Chowezanani
	Kutendwa	Chowezwa
	Kutendesha	Chowezeshea

Jedwali hilo hapo juu ni udhihirisho wenye kubainisha kuwa maneno ya Kimakunduchi yanayo mnyambuliko. Tumeona kuwa maneno 'kuvika', 'kuwapa', 'kuvwaza', 'kugwia', 'kuvita' na 'kuchowea', yote yameonyesha mnyambuliko katika kauli mbalimbali. Yamkinika hali hii ya mnyambuliko wa maneno ya kimakunduchi huathiri lugha sanifu wakati wa maongezi na hata katika masomo. Wamakunduchi hujiskia raha zaidi pale wanapotamka 'chowea' au 'chowezea' au 'chowezwa' badala ya 'sema' au 'semea' au 'semwa'. Laiti ingalikuwa lahaja yao haina mnyambuliko, ingewalazimu kuathiriwa na lugha sanifu hasa wakati wa maongezi yaliyo rasmi.

Nini tunajifunza kupitia mnyambuliko wa maneno hayo? Midamu kuna mnyambuliko, maneno ya Kimakunduchi yana mizizi ambishi, mizizi inayoambishika. Hivyo, mizizi hiyo ina sifa ya kubeba viambishi anuwai kama vile viambishi vya nafsi, viambishi vya njeo, viambishi vya urejeshi, n.k (taz. 2.2.2 & 2.2.3).

4.3.1.8 Maumbo ya Nomino za Kimakunduchi

Katika kuzichunguza nomino za Kimakunduchi imebainika kuwa ni nyingi zao ni nomino za kawaida ambazo hazitofautiani mno na nomino za lugha sanifu. Tofauti iliyoonekana kwamba kwa baadhi ya wakati, nomino za Kimakunduchi huwemo katika maumbo ya kilahaja; na hivyo kuyafanya makundi ya geli za majina kubadilika baadhi yao kwa mujibu wa kigezo cha upatanishi wa kisarufi. Tuchunguze mifano ifuatayo:

Kundi A

Mwana kagu (Mtoto ameanguka)

Wana wagu (Watoto wameanguka)

Kundi B

Mjiti ukatiki (Mti umekatika)

Mijiti ikatiki (Miti imekatika)

Kundi C

Dicho liumii (Jicho limeumia)

Macho yaumii (Macho yameumia)

Kundi D

Cheti chake chaga (*Cheti chake kimepotea*)

Vyeti vyake vyaga (*Vyeti vyake vimepotea*)

Kundi E

Uvivu umgwishi (*Uvivu umemwangusha*)

Wivu umwachisi (*Wivu umemwachisha*)

Kundi F

Konde yake ilimwa (*Konde yake imelimwa*)

Konde zake zilimwa (*Konde zake zimelimwa*)

Kundi G

Ugonjwa wake umtuu kitako (*Ugonjwa wake umemweka kitako*)

Kundi H

Kwimba kwake kunachekesha (*Kuimba kwake kunachekesha*)

Kwiba kunasikitisha (*Kuiba kunasikitisha*)

Kundi I

Mahaa vake vanafurahisha (*Mahali pake panafurahisha*)

Vyumbani mwake mnanukia (*Vyumbani mwake mnanukia*)

Kundi J

Maji yamemwagiki (*Maji yamemwagika*)

Kundi K

Chuvi isi (*Chumvi imekwisha*)

Tunapoichunguza vyema mifano iliyomo kwenye makundi hayo, tutabaini kuwa kila kundi linaweza kuunda 'kundi la ngeli' fulani. Kwa mfano, Kundi A linazaa 'KA-WA' badala ya 'YU/A-WA', Kundi B kwa 'U-I', Kundi C kwa 'LI-YA', Kundi D kwa

'CHA-VYA' badala ya 'KI-VI', Kundi E kwa 'U', Kundi F kwa 'I-ZI', Kundi G kwa 'U-YA', Kundi H kwa 'KU', Kundi I kwa 'M, VA' badala ya 'PA MU KU', Kundi J kwa 'YA' na Kundi K kwa 'T'.

Mjengeko huo wa makundi ya ngeli uliyo kinyume kidogo na mgawanyiko wa makundi hayo katika lugha sanifu, huathiri watumizi wa lugha sanifu wa Makunduchi kwa kiasi kikubwa. Hii huwafanya wanafunzi hao wakati wanapotunga sentensi zao waziingize ulahaja zaidi kuliko usanifu unaotarajiwa. Mwanafunzi hutoa sentensi kama hii ' Mtoto kanakuja' au 'Watoto wanakuja' badala ya 'Mtoto yuaja/anakuja' au 'Watoto waja/wanakuja'.

4.3.2 Tungo za Kimakunduchi

Kama tulivyoonyesha hapo awali, muambatano wa sauti ndiyo unaojenga maneno, na hivyo hivyo mfuatano wa maneno ndiyo unaounda tungo za Kimakunduchi. Hivyo, katika nukta hii tumeangalia muundo wa tungo za sentensi za Kimakunduchi katika hali zifuatazo:

4.3.2.1 Tungo Katika Hali ya Kiima na Kiarifu

Lahaja ya Kimakunduchi hubeba kiima na Kiarifu katika sentensi zake. Tunalibainisha hili kwa lengo la kudhihirisha utoshelevu wa lugha hii katika mawasiliano ya jamii hiyo ya kila siku. tuangalie mifano ifuatayo:

Jedwali Na. 12: Kiima na Kiarifu Katika Lahaja ya Kimakunduchi

	Lahaja ya Kimakunduchi	Lahaja Sanifu ya Kiswahili
1	Mnazi/wangama mbuyuni K A	<i>Mnazi umekwama kwenye mbuyu</i>
2	Uyoko/so mwakwaza K A	<i>Huyo siye aliyeanza</i>
3	Tangu amwache mkewe/amekuwa mtu ovyo K A	<i>Tangu amwache mkewe amekuwa mtu ovyo</i>
4	Anapokojoa/hunung'unika K A	<i>Anapokojoa hunung'unika</i>
5	Timu ya Nyota/ idafyu goli moja jana K A	<i>Timu ya Nyota imepata goli moja jana</i>

Sentensi Na.i – Na.v zinabainisha jinsi lahaja ya Kimakunduchi inavyobeba Kiima na Kiarifu. Hivyo, neno 'mnazi', 'uyoko', 'tangu amwache mkewe', 'akabaua' na 'timu ya nyota', ni kiima katika sentensi hizo, ilhali maneno yaliyobaki ni viarifu vyao. Tungo za Kimakunduchi zikiwa sentensi, zinajitosheleza kimaana. Mifano ya hapo juu inadhihirisha ukweli huo.

4.3.2.2 Tungo za Kimakunduchi na Upatanishi wa Kisarufi

Jambo la msingi katika tungo/sentensi, ni suala la upatanishi wa kisarufi. Tunapozichunguza tungo za lahajaya Kimakunduchi, tunaweza kubaini kwamba zinazo upatanishi huo. Kwa mfano, kupitia sentensi zilizomo ndani ya jedwali Na. 12 hapo juu, tunaweza kubaini kuwa sentensi Na.iii – Na. v, zote kwa pamoja zinabainisha upatanishi wa kisarufi. Kwa mfano, sentensi Na. iii, kiima chake

kinaonyesha matumizi ya mtu wa tatu, ambapo kitenzi cha kiarifu chake kimeanza na kiwakilishi kiambata 'ka' (katende) ambacho ndicho kiwakilishi kinachotumika kuwakilisha nafsi ya tatu (umoja) ya lahaja ya Kimakunduchi (taz. pia Jedwali Na. 5).

4.4 Matumizi ya Kimakunduchi Madarasani

Nukta hii inaongelea matumizi ya lugha darasani. Lengo ni kubainisha jinsi lahaja ya Kimakunduchi inavyotumika katika matumizi ya kila leo darasani. Mtafiti alifika eneo husika la Makunduchi na kufanya utafiti katika vipengele kadhaa vya matumizi hayo. Utafiti uliwahusu wanafunzi na walimu wao. Katika utafiti huo, mtafiti alitoa hojaji kadhaa zenye maswali yanayohitaji majibu juu ya matumizi ya lahaja hiyo darasani. Kuna sababu tatu ambazo zilimfanya mtafiti aandae hojaji kwa ajili ya wanafunzi na walimu. Kwanza, ujibuji wa hojaji ni siri ya aliyenayo. Hivyo, hutarajiwa kuwa majibu yanayotolewa ni yenye ukweli, na wala hayana ushawishi wa kumvutia mwengine kuunga mkono jibu la mwenzake. Pili, hojaji hutumia maandishi, na hivyo, ni kumbukumbu yenye kudumu na yenye urasmi. Tatu, kuwepo kwa hojaji za walimu na wanafunzi hubainisha ukweli au udanganyifu wa majibu yalitolewa.

4.4.1 Matumizi ya Lugha darasani.

Katika nukta hii mtafiti aliweza kubaini matumizi ya lugha darasani jinsi yalivyo. Alitayarisha swali lake na kuwapatia wanafunzi 90. Kati ya hao, wanafunzi 60 walitoka shule za sekondari (Kidato cha 3 na 4) ilhali 30 ni wanafunzi wa shule ya msingi na kati (Kidato cha 2). Wanafunzi wote walijibu swali hilo isipokuwa wanafunzi wanne. Swali liliulizwa hivi:

i) Wakati wa somo la Kiswahili, matumizi ya Lahaja ya Kimakunduchi huwa:

A: Makubwa sana	B: Makubwa	C: Kati na kati
D: Madogo	E: Madogo sana	F: Hakuna.
Majibu yaliku hivi:		
A → 10.4%	B → 6.9%	C → 32.5
D → 22.09%	E → 16.2%	F → 11.7%

Ni dhahiri kuwa majibu yanaonyesha kuwa kuna mchanganyiko wa matumizi ya lugha katika darasa la Kiswahili. Kiwango cha asilimia 32.5 kinapochanganywa na kile cha 'A' na 'B' kinafanya wastani wa asilimia 50. Asilimia hii (50%) inabainisha mvutano wa kimawazo ya wanafunzi wenye kukubali kuwa matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi darasani ni makubwa au madogo. Vyovyote iwavyo, matokeo haya yanaashiria kuwepo kwa utumikaji wa lahaja hiyo katika somo la Kiswahili. Kuna mihimili miwili inayoashiria matumizi hayo. Kwanza ni muhimili unaobeba kifungu 'A - B' na wa pili, wenye kubeba kifungu 'D - E' ambavyo vilimtaka mwanafunzi aseme iwapo matumizi hayo ni 'madogo' au madogo sana'. Ni asilimia 11.7 ndiyo iliyokataa kuwepo kwa matumizi ya lahaja hiyo darasani. Asilimia hii haiwezi kutumika kama kigezo cha kukana matumizi ya lahaja hiyo.

Tafsiri ya matokeo hayo: Hali hiyo inatambulisha kwamba somo la Kiswahili halina ufanisi mzuri katika mitihani ya Taifa. Dai hili linathibitishwa na matokeo ya mtihani wa Kidato cha Nne (2010) ambapo jumla ya wanafunzi 169 walijisajili kufanya mitihani ya Taifa. Kati ya hao, wanafunzi 165 waliufanya mtihani wa somo la Kiswahili; ambapo wanafunzi 40 walifaulu kupata kiwango cha 'D' na 'C' (C-3, D-47). Waliobaki, hawakufaulu (wamepata F).

Swali hilo pia liliulizwa kwa walimu, majibu yao yalikuwa hivi:

a) → 0% B) → 0% (C) → 0%
 d) → 11% E) → 33.3% (F) → 55.5%

Majibu hayo yanaashiria kuwepo kwa matumizi ya lahaja hiyo katika kiwango kidogo cha asilimia 44 tukijumlisha matokeo ya D na E, ilhali asilimia 55.5% imedhihirisha kuwa hakuna matumizi ya lahaja hiyo wakati wa somo hilo. Matokeo haya yanaashiria mvutano wa kimawazo kwa walimu hao. Wapo wanaokubali na wenye kukataa kuwepo kwa matumizi ya lahaja hiyo darasani. Vyovyote iwavyo, ingawa ni kwa asilimia ndogo, walimu nao wanakiri kuwepo kwa matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi wakati wa somo la Kiswahili.

Aidha, wakati wa somo, hakimu mzuri wa kuelewa kuwepo au kutokuwepo kwa matumizi hayo, ni mwanafunzi. Mwalimu kama ‘mwalimu’ anaweza kukataa kwa hisia za hofu ya kikazi. Asilimia kubwa ya wanafunzi waliokiri kuwepo kwa matumizi hayo yamezidi kupata nguvu ya asilimia 44 ya walimu waliyounga mkono kauli hiyo. Na bila shaka, matokeo ya Kidato cha Nne yaliyooneshwa hapo juu ni ushahidi unaokana asilimia 55 ya walimu iliyokataa kuwa kuna matumizi makubwa ya lahaja ya Kimakunduchi darasani.

4.4.1.1 Lugha ya Wanafunzi

Katika kuendeleza maswali ya hojaji, mtafiti aliweka swali jengine lililotaka kujua ni kwa kiasi gani wanafunzi huitumia lahaja yao wakati wa somo la Kiswahili. Swali lilikuwa hivi:

ii) Wanafunzi huitumia lahaja ya Kimakunduchi wakati wa somo la Kiswahili katika kiwango:

- a) Kikubwa sana (b) Kikubwa (c) Kati na kati
 (d) Kidogo (e) Kidogo sana (f) Hakuna.

Jumla ya wanafunzi 86 kati ya 90 walilijibu swali hilo. Kati yao, wanafunzi 59 walitokea shule za sekondari, wakati wanafunzi 27 ni kutoka shule ya msingi na kati.

Majibu yalikuwa hivi:

- a) → 16.2% (b) → 25.5% (c) 17.4 → 0%
 d) → 20.9% (e) → 11.7% (f) → 9.3%

Majibu hayo yanaweza kugawiwa katika makundi matatu. Kwanza, kundi lenye kukubali kuwepo kwa matumizi hayo. Kundi hilo lipo kati ya kiwango cha 'kati na kati' hadi 'kikubwa sana' (C - A) ambapo limebeba asilimia 58. Kundi la pili ni lile linaloonyesha matumizi hayo katika kiwango 'kidogo – kidogo sana'. Kundi hili limebeba asilimia 33, ilhali kundi la tatu lenye kukataa kwamba hakuna matumizi yeyote ya lahaja hiyo kwa wanafunzi hao wakati wa somo la Kiswahili, ambalo lina asilimia 9. Aidha, swali hilo limeulizwa kwa walimu wa shule za sekondari pamoja na zile za msingi na kati wa somo la Kiswahili. Jumla ya walimu hao ni 9, na majibu yao yalikuwa hivi:

- a) → 0% b) → 11.1% (c) → 22.2%
 d) → 22.2% e) → 44.4% (f) → 0%

Kupitia mtiririko huu hapo juu, kundi 'C – A' linabeba asilimia 33, kundi 'E – D' linabeba asilimia 66, ilhali kundi 'F' asilimia 0. Mgawanyo wa majibu hayo

unatudhihirishia kitu kimoja cha msingi, kwamba walimu wote wanakiri kuwepo kwa matumizi ya lahaja hiyo kwa wanafunzi wao wakati wa somo la Kiswahili. Tunajifunza nini katika kuyazingatia majibu ya wanafunzi na walimu? Kinachojitokeza hapa ni udhihirisho wa matumizi ya lahaja hiyo katika Kiswahili Sanifu. Maana, tunapoongelea somo la Kiswahili, muelekeo wetu upo katika usanifu zaidi. Hivyo basi, madamu kuna asilimia kubwa ya matumizi ya lahaja hiyo katika somo hilo, lazima kuna athari ambazo hujitokeza. Athari hizo zimebainishwa katika sura inayofuata.

Majibu ya wanafunzi yamebainisha kuwa ipo asilimia ndogo iliyodai kuwa hakuna matumizi yeyote ya lahaja hiyo wakati wa somo hilo. Yamkinika wanafunzi waliojibu hivyo hawakuwa sahihi. Kuna sababu mbili za kusema hivyo. Kwanza, wakataaji ni asilimia ndogo sana (9.3%). Pili, mwalimu ndiye hakimu mzuri wa wanafunzi na yale wayatendayo wanapokuwa darasani. Hivyo, kwa kuwa hakuna mwalimu aliyekataa, ni dhahiri kuwa majibu ya wanafunzi hao wachache, hayakuwa sahihi.

4.4.1.2 Lugha ya Walimu

Swali la tatu lilihusu lugha ya walimu ikoje wakati wa somo la Kiswahili darasani. Utafiti uliichunguza lugha hiyo kwa lengo la kuelewa iwapo lugha hiyo huambatana na matumizi ya lahaja au la. Swali lilikuwa hivi:-

- iii) Walimu huitumia lahaja ya Kimakunduchi wakati wa somo la Kiswahili katika kiwango:
- | | | |
|-----------------|-----------------|------------------|
| a) Kikubwa sana | (b) Kikubwa | (c) Kati na kati |
| d) Kidogo | (e) Kidogo sana | (f) Hakuna. |

Swali lilijibiwa na idadi ya wanafunzi 87 kutoka shule za Sekondari na Msingi na Kati, na pia kwa walimu wa shule hizo. Majibu yalikuwa kama ifuatavyo:

i) Majibu ya walimu

a) → 0% b) → 0% (c) → 0%
 d) → 0% e) → 55.5% (f) → 44.4%

ii) Majibu ya wanafunzi

b) → 10.4% b) → 8.1% (c) → 19.7%
 d) → 27.9% e) → 20.9% (f) → 13.9%

Tunapoyachunguza majibu ya walimu, tunabaini kuwa wapo baadhi yao wanaokiri kuwepo kwa matumizi hayo ingawa kwa kiwango kidogo sana. Tumeona kuwa asilimia 55.5 imekiri kuwa walimu huitumia lahaja hiyo wakati wa somo la Kiswahili katika kiwango kidogo sana. Asilimia hii ni kubwa ambayo inadhihirisha kuwepo kwa matumizi hayo. Aidha hatua hiyo ya kukiri japo kwa kiwango kidogo sana inaweza kuchukuliwa kama kigezo cha kukataa mawazo ya walimu waliyosema hakuna matumizi hayo. Kwa mawazo yetu tunaona kwamba walimu walipinga kuwepo kwa matumizi ya Kimakunduchi darasani wakichelea kujidhalilisha kwamba wanashindwa kutumia Kiswahili Sanifu darasani na hivyo hawaimudu kazi yao vizuri.

Majibu ya asilimia 55.5 ya walimu kwamba wanatumia lahaja hii kwa kiwango kidogo yamepata nguvu za majibu ya wanafunzi yanayoonyesha kuwepo kwa matumizi hayo ya lahaja wakati wa somo la Kiswahili. Yanapochunguzwa kwa kina majibu ya wanafunzi hao, tunaona kuwa ni asilimia 14 pekee ndiyo iliyokataa

kwamba walimu hawatumii lahaja hiyo wakiwa darasani. Asilimiya 86 imekiri kuwepo kwa matumizi hayo ingawa katika viwango tofauti. Kati ya kiwango hicho, asilimia 38 ni wanafunzi waliyosema kuwa walimu wanaitumia lahaja hiyo baina ya kiwango cha 'kati na kati' na 'kikubwa sana', ilhali asilimia 48 imeonyesha kuwa maumizi hayo yapo kati ya kiwango 'kidogo na kidogo sana'.

Tafsiri ya matokeo haya ni ipi? Maelezo yanamaanisha kwamba walimu wakiwa nao ni Wamakunduchi wanashindwa kuyadhibiti matumizi ya lahaja yao wakati wanapofundisha masomo yao likiwemo somo la Kiswahili. Jambo hili hupelekea wanafunzi kutokuwa mahiri katika matumizi ya Kiswahili Sanifu kwa sababu walimu wao wanatumia Kimakunduchi na wanafunzi nao pia wanatumia lahaja hiyo katika kujifunza darasani. Ndiyo maana matokeo ya mitihani yao huonekana hafifu, siyo kwa somo la Kiswahili pekee, hata katika masomo mengineyo. Iwapo tunarejelea matokeo ya mitihani ya Taifa ya mwaka 2010 tunaonakuwa wanafunzi 169 walijisajili kuifanya mitihani hiyo. Kati ya hao, ni mwanafunzi mmoja pekee aliyepata 'Daraja la Kwanza'. Wanafunzi 29 wamekosa vyeti na waliyobaki, wamepata daraja la tatu na nne (Daraja la Tatu-13 na la Nne-122). Chanzo cha kuanguka daraja zao ni wanafunzi wengi kufeli katika somo la Kiswahili.

4.4.2 Matini za Walimu

Mtafiti aliomba matini za kufundishia kutoka kwa walimu wa somo la Kiswahili. Lengo ni kuzichunguza iwapo zinatumia lugha sanifu au la. Walimu wote walimpatia mtafiti matini hizo. Matini hizo zilihusu 'dhana ya fasihi pamoja na kubainisha tofauti zinazojitokeza kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi', 'uhakiki wa ushairi', 'methali', 'matumizi ya lugha', 'ukuaji na uenezaji wa Kiswahili enzi ya

Waingereza', 'Asili ya Kiswahili' na pia alipewa 'andalio la somo'. Matini zote hizo zimebainika kutumia Kiswahili Sanifu. Matini hizo zimeambatanishwa nyuma.

Hali hii inadhihirisha kuwa katika maandishi ya walimu mara nyingi hakujitokezi matumizi ya lahaja yao. Kuna sababu za matini hizo kuwepo katika hali hiyo. Kwamba kanuni ya ufundishaji inalazimisha kutumika lugha sanifu katika maandishi. Kinyume chake, ni kosa la mwalimu kutumia lahaja yake katika maandishi yaliyo rasmi. Aidha, matini, hizi zimebainika kuwa kwa asilimia kubwa ni maandishi sanifu yaliyonukuliwa katika vitabu husika vya mada iliyokusudiwa kufundishwa. Kwa mfano, iwapo mada ilihusiana na 'Historia ya Kiswahili' mara nyingi maelezo yake huchukuliwa katika vitabu vilivyoelezea historia hiyo. Hivyo hivyo, na iwapo mada iliyokusudiwa ilihusu matumizi ya lugha, maelezo yake huchukuliwa kitabuni katika kiwango kikubwa. Katika utafiti huu zilipatikana matini nane kati ya tisa. Matini zote hizo zimefungamana na urasmi, bila ya kuona ulahaja hata kwa asilimia ndogo. Hii inatubainisha kuwa uwezo wa walimu wa kufundisha kwa lugha rasmi/sanifu upo. Isipokuwa hukosekana kutokana na taathira za kimazoea ya kimaongezi. Kwa bahati mbaya, maongezi yanaathiri zaidi kuliko maandishi. Na hii ndiyo iliyopelekea wanafunzi na hata walimu kukiri kuwa lahaja hiyo hutumika wakati wa somo la Kiswahili.

4.4.2.1 Lugha ya Muhtasari wa Masomo

Kwa kawaida muhtasari wa masomo huandaliwa na Wizara ya Elimu ambayo ndiyo chombo pekee cha Serikali chenye mamlaka ya kufanya hivyo. Hakuna muhtasari unaoandaliwa na shule wala taasisi nyengine isipokuwa taasisi ya mitaala ya wizara hiyo. Utaratibu wa kuandaliwa muhtasari huo na taasisi moja una lengo moja

mahsusi la kimsingi. Kwamba, kusiwe na utofauti wa mada zinazosomeshwa kati ya shule moja na nyingine ili kuwafanya wanafunzi wote wawe katika kiwango kimoja cha elimu.

Aidha, muhtasari unapoandaliwa na taasisi moja pekee huwafanya watahini wapate urahisi wa kuwatahini wanafunzi wote. Kwamba, muhtasari ndiyo unaowaelekeza waanze wapi katika utangulizi wa mitihani, na wamalizie wapi. Laiti kama kila shule, wilaya na hata mkoa, kuna mihutasari tofauti, bilaya shaka, kungekuwa na ugumu katika utungaji wa mitihani ya Taifa. Pia, muhtasari huwaunganisha wanafunzi kuwa kitu kimoja, na hivyo, wanafunzi wa shule tofauti wanao uwezo wa kusaidiana katika mijadala yao ya kimasomo. Kimuhtasari, umuhimu wa muhtasari wa namna moja ni mwingi, na wala hakuna haja ya kuuwasilisha hapa. Jambo la kuzingatia, ambalo limebainika na utafiti huu, kwamba muhtasari wa somo hili, hauna hata nukta ndogo ya ulahaja. Bila shaka, kuna sababu za kimsingi za muhtasari kuwa katika hali hiyo. Ni vyema tukaziorodhesha japo chache kama hivi ifuatavyo:

- Muhtasari ni dira ya walimu na wanafunzi wote wa Tanzania. Si urahisi kutumia lahaja yeyote kwa vile Kiswahili chenye kuwaunganisha wanafunzi na walimu wao, ni kila chenye urasmi. Hivyo, ni lazima muhtasari huo utumie lugha sanifu.
- Somo linalofundshwa hutakiwa lifuate kanuni za usanifu. Hivyo, kiini cha usanifu huo lazima kianze kwenye muhtasari.
- Katika lugha ya Kiswahili, kuna lahaja na lugha nyingi za makabila. Iwapo kutalazimika kutumia lahaja, itashindikana kuamua ni lahaja ipi

itumike, maana kila lahaja itapenda itumiwe katika muhtasari huo. Tena, athari ya matumizi ya lahaja hiyo itakuwepo kwa wanafunzi na walimu waliyo wengi Tanzania. Kwamba kila kipindi kifupi ni lazima kuwe na semina au warsha za kuwaelekeza wanafunzi na walimu makusudio yale yaliyomo katika muhtasari huo.

4.4.2.2 Kazi za Wanafunzi

Mtafiti alichunguza kazi za wanafunzi ili abaini iwapo kuna matumizi ya lahaja hiyo au la. Kazi zilizochuguzwa ni za aina mbili. Kwanza, utungaji wa insha, ilhali ya pili, ni utungaji wa sentensi fupifupi zilizoongozwa na maneno maalum. Hebu tuangalie kipengele kimoja kimoja.

a) Utungaji wa Insha

Katika kuzichunguza insha za wanafunzi 86 wa shule za sekondari na msingi na kati, mtafiti amebaini matatizo anuwai. Baadhi ya matatizo hayo ameyabainisha hapa; si kwa nia mbaya, ila kwa nia ya kuwatanabahisha wale wasomaji wa kazi hii, hususani walimu na wahusika wa mitaala, kwamba kunahitajika juhudi kubwa kwa wanafunzi wa ngazi hizo katika mada za utungaji. Ingawa si kusudio la utafiti huu kubainisha matatizo mbalimbali yasiyo ya kilahaja, bali mtafiti amehisi kuwa ni vyema kuyadhihirisha ili yaweza kufanyiwa kazi na wahusika, hasa walimu mashuleni.

Moja ya matatizo hayo ni kasoro za matumizi ya vituo. Yaani, wanafunzi waliyo wengi wameshindwa kutumia vituo ipasavyo katika utungaji wao. Vituo vilivyokusudiwa na kazi hii ni zile alama zenye kutumika katika maandishi ili

zimwezeshe msomaji wa kazi husika aelewe wapi pa kusita kidogo, pa kusita sana, pa kushangaa, pa kuuliza, na kadhalika. Hivyo msomaji makini wa insha hizo angeweza kubaini kuwa zina tatizo hilo, tena katika kiwango kikubwa. Tatizo la ukosefu wa matumizi ya vituo lina taathira kubwa. Kwanza hupunguza uelewa wa kazi husika, na pili, huweza kusababisha utatanishi wa maana ya baadhi ya vipengele.

Aidha, katika suala la vituo, huenda pamoja na matumizi ya uandishi wa maneno. Yaani, kuna nyakati ambazo mtu hulazimika aanze neno lake kwa herufi kubwa hususani, mara baada ya kuwepo kwa kituo kikubwa (kitojo), au majina ya siku, majina ya pahala, na hata majina ya watu. Kwa bahati mbaya, wapo wanafunzi waliyo wengi ambao wameshindwa kuutumia ujuzi huo.

Tatizo lingine ni matumizi ya lahaja. Yaani, jinsi lahaja inavyotumika katika utungaji wao wa insha. Mtafiti amebaini kuwa yapo baadhi ya matatizo ya kimsamiati yaliyomo ndani ya insha hizo. Utafiti umeweza kubaini maneno kama vile ‘kunako masomo’ badala ya ‘*kwenye masomo*’ ‘walinishukuwa’ badala ya ‘*walinichukuwa*’ ‘nipata kukosa’ badala ya ‘*nimepata kukosa*’, ‘singo’ badala ya ‘*shingo*’ ‘ninalala’ badala ya ‘*ninalala*’ ‘nilifulahi’ au ‘niliwashukulu’ badala ya ‘*nilifurahi*, au ‘*niliwashukuru*’, ‘kufauru’ badala ya ‘*kufaulu*’ na ‘mwalimu awapo’ badala ya ‘*mwalimu anapokuwepo*’. Hiyo ni mifano ya baadhi ya misamiati ya kilahaja iliyomo ndani ya insha hizo. Hata hivyo, mtafiti hakuweza kubaini makosa mengi ya kimsamiati. Tathmini yake katika makosa hayo ni asilimia 25. Hata hivyo, asilimia hiyo si ndogo, ni kubwa hususani ikizingatiwa kwamba uandishi wa insha unahitaji lugha iliyo sanifu tu. Kuibuka kwa misamiati ya kilahaja husababisha

upungufu wa uelewa wa insha husika, na hivyo, kumfanya mtahini wa mitihani ya Taifa atoe alama pungufu. Kupata alama pungufu kwa mwanafunzi kuna madhara. Maana, yamkinika kwamba badala ya kupata kiwango cha 'A' akapata 'B'. Jambo hili humpunguzia sifa zake za ufaulu katika uwanja wa taaluma.

Kwa upande mwingine, mtafiti alitoa maneno kadha katika hojaji zake ili yaweze kutungiwa sentensi na wanafunzi hao. Maneno yaliyotolewa ni 'kula' na 'cheza' ambapo mwanafunzi alitakiwa atumie njeo ya 'wakati wa sasa' (-na-), kwa neno 'imba' na 'soma', atumie njeo ya 'wakati uliopita – muda mrefu' (-li-), kwa neno 'uza' na 'nunua' na 'sema' na 'sikiliza' kwa 'wakati ujao', na neno 'lima' na 'vuna' kwa 'hali ya mazoea'.

Katika maneno hayo, mwanafunzi alielekezwa ayatungie sentensi katika lahaja ya Kimakunduchi, na kisha, azifasiri sentensi hizo katika Kiswahili Sanifu. Kwa bahati njema, wanafunzi wote 86 waliweza kutunga sentensi katika hali zote mbili. Majibu yaliyojitokeza yaligawika katika hali tatu. Moja, majibu sahihi yenye usanifu na urasmi, pili, majibu fasaha yasiyo sanifu wala urasmi, na tatu, majibu yaliyomezwa na ulahaja.

a) Majibu Sahihi yenye Usanifu na Urasmi

Majibu haya yametolewa na wanafunzi ambayo yamefuata taratibu zote za kisarufi. Yaani yamejibiwa kwa mujibu wa njeo iliyotakiwa, yametumia nafsi sahihi iliyoshikamana na kiambishi awali cha kitenzi, na sentensi hizo zilibaki katika upatanisho wa kisarufi, pamoja na kuleta maana iliyokusudiwa. Mfano wa sentensi hizo ni:-

- i) Mjomba amekula nanasi
- ii) Kwanini unacheza mpira?
- iii) Nimeimba nyimbo vizuri sana
- iv) Nimesoma kwa makini
- v) Kaka aliuza machungwa yake
- vi) Dada alinunua mchele
- vii) Utasema?
- viii) Utasikiliza
- ix) Ali hulima
- x) Asha huvuna

Sentensi hizo zinaashiria kitu kimoja cha msingi kwamba, licha ya dosari za baadhi ya sentensi za wanafunzi wengine, wapo baadhi yao ambao wapo makini katika matumizi sahihi ya sarufi. Hii inatufahamisha kuwa si wanafunzi wote wenye kuathirika na lahaja ya Kimakunduchi wakati wa masomo yao.

b) Majibu Fasaha yasiyo Sanifu wala Rasmi

Sentensi nyengine zilibainika kuwa na ufasaha, lakini hazina urasmi. Neno ufasaha hapa linaashiria kueleweka kwa sentensi hizo, na labda, kuwa na ukurubifu wa urasmi. Mfano wa sentensi hizo ni kama vile:

- i) Mimi nacheza
- ii) Mimi nakula
- iii) Ashasoma
- iv) Nishauza

Mifano hiyo inaashiria jambo moja kuu. Kwamba, baadhi ya wanafunzi wanahisi kuwa neno ‘nakula’ au ‘nacheza’ ni sanifu, ilhali siyo sahihi. Usahihi wake ni kusema ‘ninakula’ au ‘ninacheza’.

c) Majibu yasiyo Sahihi Kabisa

Mtafiti amebaini kuwa majibu mengi yasiyo sahihi kabisa yamejitokeza kwenye njeo ya hali ya mazoea. Hebu tuangalie mifano ifuatayo

- i) Lima (njeo ya mazoea) – Naenda kulima kondeni
 - Anakuwa analima
 - Kaka analima huko shambani
 - Hulima mama kesho
- ii) Vuna (njeo ya mazoea) – Anakuwa anavuna
 - Leo siendi kuvuna
 - Kila siku anaenda kuvuna

Mifano hiyo inabainisha waziwazi kuwa wanafunzi hao hawaelewi njeo ya mazoea ni ipi, wala matumizi yake. Katika hali hii, mwanafunzi anaweza kuanguka kwenye mitihani yake kwa tatizo hilo.

d) Majibu yenye Ulahaja

Mtafiti amebaini kuwa baadhi ya majibu yana ulahaja wa Kimakunduchi. Tuangalie mifano ifuatayo:-

- i) N’nakula
- ii) N’nacheza
- iii) Kanacheza
- iv) N’tasikiliza
- v) Niliuzu

Kwa kweli majibu hayo yanadhihirisha athari za ulahaja kwa wanafunzi hao. Kama uandishi na ujibuji wa maswali ya mitihani unachukua sura hiyo, inamaanisha kuwa ufaulu wao katika somo la Kiswahili pia utakuwa duni.

4.5 Athari za Kimakunduchi kwa Kiswahili

Katika nukta hii mtafiti amebainisha athari mbali mbali za lahaja ya Kimakunduchi kwa Kiswahili Sanifu. Athari hizo zimedhihirika wakati wa ukusanyaji wa data katika shule ambazo mtafiti alifika. Athari zinaweza kuwa hasi au chanya. Hata hivyo nyingi ya athari zilizobainika, ni hasi. Hivyo, katika nukta hii zilichunguzwa athari za kiisimu, pamoja na kuzingatia athari kwa utoaji wa elimu, na ni zipi taathira ya athari hizo.

4.5.1 Athari za Kiisimu

Katika nukta hii, utafiti umebainisha athari za kiisimu kwenye sauti, kwenye maneno, kwenye tungo. Ni vyema kabla ya kuzibainisha athari zenyewe, tuchunguze maana ya isimu. Hartman (1972) akinukuliwa na Mgullu (2001) anasema, 'Isimu ni eneo maalumu la mtalaa ambalo lengo lake huwa ni kuchunguza lugha.' Nayo TUKI (2004) imeifasili dhana hiyo kama, 'Taaluma inayochunguza na kuchambua lugha kisayansi'.

Fasili hizo zimekuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu, kwa misingi kwamba zimesaidia katika kumwongoza mtafiti kuelewa kuwa uchambuzi wa lugha unahitaji usayansi wa hali ya juu. Bila shaka, wataalamu mbalimbali wanaungana katika kukubali kuwa kipengele cha sauti, uchambuzi wa neno na hata tungo, kwa pamoja

ni mwenendo mzima wa kiisimu. Sasa tuangalie ni athari zipi zilizobainika katika kila kipengele kilichodhihiri hapo juu.

4.5.1.1 Athari katika Sauti

Katika maswali yaliyomo katika hojaji ya wanafunzi na ya walimu limo swali kuhusiana na sauti. Swali lenyewe ni hili:

- i) Kiswahili sanifu huathiriwa na sauti za lahaja ya Kimakunduchi katika kiwango:-

- | | | |
|-----------------|-----------------|------------------|
| A: Kikubwa sana | (b) Kikubwa | (c) Kati na kati |
| d) Kidogo | (e) Kidogo sana | (f) Hakuna. |

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 86 kati ya 90 waliyotarajiwa kulijibu, na pia lilipata majibu ya walimu wote waliotafitiwa. Sura ya majibu yao ilikuwa hivi:-

- a) Majibu ya wanafunzi

- | | | |
|------------|------------|-------------|
| a) → 5.8% | b) → 15.1% | (c) → 16.2% |
| d) → 19.7% | e) → 18.6% | (f) → 13.9% |

- b) Majibu ya walimu

- | | | |
|------------|------------|-------------|
| a) → 44.4% | b) → 11.1% | (c) → 11.1% |
| d) → 0% | e) → 33.3% | (f) → 0% |

Tunapoyachunguza majibu ya wanafunzi tunabaini kuwa asilimia 86 inakiri kuwa zipo athari za matumizi ya sauti za lahaja ya Kimakunduchi katika somo la Kiswahili. Tumeona kuwa asilimia 37 (a – b) inadhihirisha kuwepo kwa matumizi kati ya 'makubwa sana' na 'kati na kati', asilimia 39 inakiri kuwepo kwa athari hizo kwa kiwango kilicho baina ya 'kidogo' na 'kidogo sana' ilhali asilimia 14 imesema

hakuna athari hizo. Kazi hii haiwezi kukataa maoni ya wanafunzi waliokataa, bali, kwa kuzingatia maamuzi ya wanafunzi walio wengi, tunaweza kukubali kuwa athari hizo zipo. Kiwango cha asilimia 37 kinakaribiana kuwiana na kiwango cha asilimia 39. Hii inatoa taswira kwamba athari za matumizi hayo ya sauti wakati wa somo la Kiswahili ni ya kati na kati.

Kwa upande wa majibu ya walimu, nayo yanaashiria kuwepo kwa athari za matumizi hayo, tena kwa kiwango kikubwa sana. Yaani, walimu wote wamekiri kuwa zipo athari hizo, tena athari zenyewe ni kubwa. Tunaporejlea 'A – C', utaona kuwa katika kiwango hicho, kuna asilimia 66 ya waliokubali, ambapo kiwango hicho kinawakilisha kati ya athari zilizo 'kubwa sana' na 'kati na kati.' Majibu haya pekee yanatufahamisha kuwa nguvu ya athari ya sauti za Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu ni kubwa mno. Tuna sababu tatu za kusema hivyo. Kwanza, watafitiwa wenye kukubali kuwapo kwa athari hizo za sauti ni walimu. Vyovyote iwavyo, walimu hawawi sawa na wanafunzi. Kauli yao (hasa katika nukta kama hii) hupewa nguvu kwa vile wao ndiyo watambuzi wa mambo. Pili, walimu ni waajiriwa wa serikali. Mara nyingi huficha mambo japo yana ukweli. Iwapo hiyo ndiyo hulka yao, kwanini tukatae waliyoyakiri na ilhali madhara ya kubainisha ukweli huo yanaweza kuwasibu wenyewe? Bila shaka, walichosema ni sahihi, na wamesema kwa kujiamini, na hususan kwa vile hakuna ubaya wowote katika utafiti kukiri jambo lililo 'ndilo'. Kinyume yake ni hiyana na dosari kwa mtafitiwa kuficha yaliyo na ukweli kwa kuchelea madhara fulani. Tatu, idadi ya walimu hao waliyokiri ni asilimia 100. Kwa msingi huu mtafiti anaamini kuwa zipo athari za sauti za Kimakunduchi katika matumizi ya kila leo kwa Kiswahili Sanifu.

Ingawa tumegusia kuwa athari hizo zinaonekana zaidi katika maongezi, lakini ni dhahiri kuwa madhara yake yanamalizia kwenye maandishi. Na hii ndiyo maana wakati tunaongelea matumizi ya kilahaja katika somo la Kiswahili kwa wanafunzi na walimu, wote, kwa pamoja walikiri kuwepo kwa matumizi hayo (rejea 3.1.1 na 3.1.2).

4.5.1.1 Athari katika Maneno

Kiambatanisho I na IV vinaonyesha swali lililoulizwa kwa wanafunzi na walimu kuhusu jinsi maneno ya Kiswahili Sanifu yanavyoathiriwa na lahaja ya Kimakunduchi. Swali lilikuwa hivi:

- i) Maneno ya Kiswahili Sanifu huathiriwa na lahaja ya Kimakunduchi katika kiwango:-
- | | | |
|-----------------|-----------------|------------------|
| a) Kikubwa sana | (b) Kikubwa | (c) Kati na kati |
| d) Kidogo | (e) Kidogo sana | (f) Hakuna. |

Lengo la swali hilo lilikuwa kuchunguza iwapo lahaja ya Kimakunduchi inayaathiri maneno ya Kiswahili Sanifu. Hebu tuangalie majibu yaliyotolewa na wanafunzi 86 wa shule tatu za Makunduchi pamoja na majibu yaliyotoka kwa walimu wa somo la Kiswahili wa shule hizo.

- ii) Majibu ya wanafunzi
- | | | |
|------------|------------|-------------|
| a) → 13.9% | b) → 13.9% | (c) → 11.7% |
| d) → 34.8% | e) → 18.6% | (f) → 8.1% |
- ii) Majibu ya walimu
- | | | |
|------------|------------|-------------|
| a) → 0% | b) → 33.3% | (c) → 11.1% |
| d) → 33.3% | e) → 22.2% | (f) → 0% |

Majibu ya wanafunzi yanajitokeza katika sura tatu. Sura ya kwanza yanaonekana katika kifugu 'A – C' kinachowakilisha kiwango kilicho baina ya ‘kikubwa sana’ na ‘kati na kati’. Majibu haya yamechukua jumla ya asilimia 40. Sura nyengine ni ile ya 'D – E' ambayo imebainisha athari hizo katika kiwango ‘kidogo' hadi ‘kidogo sana’, ambapo hapa pana jumla ya asilimia 54, na mwisho, sura ya ‘F’ inayowakilisha dhana ya kukataa kuhusu kuwepo kwa athari hizo. Katika sura hii kuna jumla ya asilimia 8. Majibu haya ya wanafunzi yameashiria wazo moja kuu. Kwamba, zipo athari za kiisimu zinazojitokeza katika maneno ya Kiswahili Sanifu. Hapa tunaziangalia athari hizo katika hali mbili. Nazo ni ‘hali ya umbo lenyewe’, na pili, 'ulahaja uliojitokeza katika neno husika'.

a) Hali ya Umbo Lenyewe la Neno

Data zimeonyesha kuwa baadhi ya wanafunzi, wameathirika na maneno ya kilahaja na hivyo, ule usanifu wa neno husika hukosekana. Ipo mifano mingi iliyotolewa na wanafunzi hao wakati walipotakiwa watunge sentensi sanifu kutokana na na maneno waliyopewa. Mathalani, tuangalie majibu ya usanifu wa wanafunzi hao kwa maneno waliyopewa.

Maneno Waliyopewa

Majibu Yao

Kula

nakula

Cheza

nacheza

Soma

ashasoma.

Hiyo ni mifano ya majibu yao. Bila shaka inaeleweka wazi kuwa umbo la neno sanifu, kwa kawaida hubeba viambishi vine vilivyo sanifu. Ambavyo ni kiambishi

nafsi, kiambishi cha njeo, mzizi wa neno, na kiambishi cha mnyambuliko. Kinyume na kuwemo mambo hayo, na kinyume na neno lenye umbo la hali ya amri, neno hilo hutafsirika kuwa lina upungufu wa kiisimu/kisanifu. Kama ni hivyo, maneno ya hapo juu, ima yana upungufu wa kiambishi, hususan kiambishi cha nafsi kama ‘nakula’ badala ya ‘*ninakula*’ au ‘nacheza’ badala ya ‘*ninacheza*’. Au yana ulahaja uliosababisha kupotea kwa usanifu. Mfano, ‘n’nakula’ badala ya ‘*ninakula*’ au ‘nnachecha’ badala ya ‘*ninacheza*’ au ‘ashasoma’ badala ya ‘*amesoma*’. Je, iwapo utaratibu wa kiisimu haukufuatwa ipasavyo katika neno, kuna madhara gani?

Kama tulivyosema hapo awali, isimu ni sayansi ya lugha. Bila shaka neno ‘usayansi’ hunasibishwa na hatua maalum zenye kumlazimu mtafiti kuzipitia katika mpangilio wake huo huo. Kutozifuata ipasavyo, mara nyingi husababisha kupata majibu yenye utatanishi; au yasiyo sahihi. Hivyo, tunapoyarejelea majibu ya maneno ya hapo juu ya wanafunzi, tunabaini kuwa ule usahihi uliyofasaha, unakoseka. Kwa mfano, neno ‘nakula’ au ‘nacheza’ yanakosa usahihi wa kunasibishwa na nafsi fulani. Yaani, je maneno hayo yanahusishwa na nafsi ipi? Mfano, mimi, wewe, sisi, nyinyi, yeye au wao? Mfano mimi nakula, sisi nakula, wewe nakula, nyinyi, nakula, n.k.

Aidha, kwa kukosa usahihi wa kunasibishwa na nafsi fulani, dhana ya ukosefu wa upatanishi wa kisarufi nayo inajitokeza. Yaani, mtu anaposema ‘mimi nakula’ au ‘wewe nakula’, kwa wanaisimu watajiuliza, ‘kiko wapi kiambishi’ kinachodhihirisha matumizi ya nafsi kwenye vitenzi hivyo? Kama hivyo ndivyo, dhana ya utatanishi pia inadhihirika.

Neno ‘ashakuja’ nalo linachukua sura kama hiyo ya utatanishi. Utatanish uliopo hapa ni wa kinjeo. Kiambishi –sha- hutumika kama kisaidizi cha njeo ‘– me-‘ na ‘- li -’. Hivyo, inapotumika peke yake, mwanaisimu anashindwa kuelewa iwapo tendo la kuja limefanyika kwa muda mfupi uliopita au mrefu, na hivyo kusababisha kupotea kwa maana fulani.

b) Hali ya Ulahaja Iliyojitokeza katika Maneno

Ulahaja unapojitokeza katika neno, hujitokeza athari za kiisimu katika neno husika. Kwa mfano, mwanaisimu anapoliona neno ‘nnakula’ au ‘nnacheza’, hujiuliza, je, mfuatano wa ‘n’ mbili (nn) huashiria sauti moja kama ilivyo kwa /ny/, (kw/ na /mw/, au ni sauti mbili tofauti? Na je, ‘nn’ hizi ni mofimu moja kama ilivyo kwa ‘-som-’, ‘-chek-’ na ‘-f-‘ au ni mofimu mbili tofauti zenye majukumu yaliyo tofauti? Hivyo, msingi wa maswali hayo ndiyo unaopelekea kuzuka kwa utatanishi wa tafsiri ya uchambuzi wa kazi za viambishi/mofimo zinazojitokeza katika maneno hayo. Tafsiri ya kazi za kila mofimu ya neno ni muhimu sana. Ndio inayoongoza katika kuleta maana sahihi iliyokusudiwa. Ingawa hivyo, kwa upande wa isimu ya lahaja ya Kimakunduchi, hakuna kosa kutamka au kuandika kama ilivyojitokeza hapo juu.

Madhara ya athari hizo yapo katika ukosaji wa natija nzuri kwa mwanafunzi. Ni dhahiri kuwa mtahini wa mitihani ya Taifa hawezi kumpatia alama mwanafunzi ambaye atakwenda kinyume na usahihi uliowekwa wa mwongozo wa usahihishaji aliopewa. Na bila shaka, muongozo wa usahihishaji hauwezi kukubaliana na uandishi wa namna hiyo. Yamkinika hali hii ya kuwepo kwa athari za kilahaja katika maumbo ya maneno ya Kiswahili Sanifu ndiyo yanayopelekea wanafunzi kuanguka katika mitihani yao ya Taifa. Mtafiti amejaribu kuchunguza pia matokeo ya mitihani

wa Taifa ya mwaka 2009 kwa wanafunzi wa shule ya Makunduchi. Amebaini kuwa kati ya wanafunzi 55 waliyofanya mtihani wa Kiswahili, wanafunzi 13 walilifeli somo hilo. Idadi hiyo ni ndogo kimtazamo, lakini kimazingira ni kubwa. Inabeba karibu ya asilimia 28. wakati wanafunzi hao hao wameweza kufaulu somo la Dini ya Kiislamu kwa asilimia 98, somo la Uraia (civics) kwa asilimia 84, somo la Kiarabu kwa asilimia 98 na somo la Kiingereza kwa asilimia 67. Inaeleweka kuwa Wazanzibari wanaielewa zaidi lugha yao mama ya Kiswahili kuliko hata Dini ya Kiislamu, au lugha ya Kiarabu. Inakuwaje, masomo hayo wawe wamefaulu vizuri zaidi kuliko somo la lugha iliyowazaa? Kimantiki, isingewezekana kufeli namna hiyo. Hapa ndipo mtafiti anapobaini kuwa yawezekana chanzo cha kuanguka kwa asilimia 28 ya somo la Kiswahili, ni athari za ulahaja unaojitokeza katika maumbo ya maneno. Aidha, ilitarajiwa wanafunzi hao waanguke sana katika somo la Kiingereza kwa vile ni lugha yao ya tatu. Lakini, hivyo sivyo ilivyokuwa. Lazima tukiri kuwa wakati wa usahihishaji wa somo lolote lile, kuna mambo kadhaa huchunguzwa. Kwa mfano, katika somo la Kiswahili hasa sarufi, huzingatiwa vipengele kama vile matumizi ya vituo na alama, upatanisho wa kisarufi na usahihi wa mambo na mpangilio wa maumbo hayo katika sentensi. Mambo kama hayo yasipofuatwa kwa makini, mwanafunzi anaweza kuanguka kinatija.

4.5.1.2 Athari katika Tungo

Dhana ya tungo ni pana, na hivyo hukusanya mambo matatu makubwa. Tungo kirai, tungo kishazi na tungo sentensi. Utafiti huu haukuzingatia maana ya aina ya dhana hizo kwa kina. Isipokuwa umejhusisha zaidi na mantiki ya dhana hizo ili msomaji aweze kubaini kwa muhtasari athari za kiisimu za lahaja ya Kimakunduchi

zilizojitokeza ndani ya tungo za Kiswahili Sanifu. Athari hizo zimejitokeza zaidi katika kazi mbili walizopewa wanafunzi wa sekondari wa shule husika. Kazi zenyewe ni insha na utungaji wa sentensi.

4.5.1.2.1 Tungo Kirai

Kirai kama ufafanuzi wa wataalamu wengi, ni aina ya utungo wa maneno usiyohusishwa na kiima kiarifu. Yaahivyioni, ufahamu wa wataalamu wengine, kirai huwa hakihusishwi na dhana ya utendaji, na hivyo, ni neno au kifungu cha neno kisichozingatia utendaji ndani yake. Katika kuzichunguza kazi za insha za wanafunzi hawa, mtafiti amebaini baadhi ya makosa madogo madogo yaliyo ndani ya vikundi virai vya maelezo yao. Ni vyema tukayadhihirisha makosa yenyewe.

Tuchunguze vifungu vifuatavyo:-

- i) ~ mitindo mbali mbali za wazungumzaji ~
- ii) ~ lugha kimazungumzo na matumizi ~
- iii) ~ yaani historia hiyo kuwa ya kwamba ~
- iv) ~ na wala pia awe na ~

Kwa muhtasari tunaweza kusema kwamba hivyo ni vikundi virai. Vikundi hivyo vimepatikana kutokana na insha za baadhi ya wanafunzi wa shule ya Makunduchi. Kama tutakuwa makini, tunaweza kubaini baadhi ya makosa ya kiisimu yaliyojitokeza ndani ya kila kifungu. Kwa mfano, katika kikundi cha mwanzo, kuna dosari ya upatanishi wa kisanifu. Yaani, neno ‘mitindo’ halichukuwi kihusishi ‘za’ na badala yake hufuatana na kihusishi ‘ya’. Hivyo, kiisimu, kifungu hicho kina

kasoro na hivyo kumfanya mtahiniwa aweze kuadhibiwa kwa kunyimwa alama iliyo nzuri.

Aidha, kifungu cha pili kina ukosefu kama huo (mtiririko wa upatanishi wa kisarufi). Iwapo neno ‘mazungumzo’ limeanza na kiambishi ‘ki’ na kuwa 'kimazungumzo', ilipasa neno ‘matumizi’ nalo lifuate utaratibu huo huo, na hivyo, kifungu hicho kilitakiwa kesomeke hivi:

~ lugha kimazungumzo na kimatumizi~

Tunapochunguza kifungu cha tatu, tunabaini kuwa kuna mtiririko wa maneno yasiyohitajika kuwepo pamoja. Kwa mfano, ‘kuwa ya kwamba’, na badala yake lilitakiwa litumike ima neno ‘kuwa’ au ‘kwamba’.

Hivyo, kifungu hicho kilitakiwa kesomeke hivi:

~yaani, historia hiyo kwamba ~ AU

~ yaani historia hiyo kuwa ~

Aidha, kifungu cha mwisho kina mtiririko kama kifungu na (iii). Kwamba kina mtiririko wa maneno yasiyo na utaratibu muafaka. Kwa mfano, neno ‘wala’ na ‘pia’ yasingelihatijika kuwepo pamoja. Pia, neno ‘wala’ halikubaliani na neno ‘awe’ na badala yake hufuatana na ‘asiwe’. Kwa ufupi vifungu hivyo vimejengeka zaidi kimazungumzo kuliko kiusanifu. Mwelekeo huo si mzuri kwa wanafunzi ambao siku za mbele wanataraji kuukabili mtihani wa Taifa wa Kiswahili. Sasa tuangalie tungo kishazi.

4.5.1.2.2 Tungo Kishazi

Kishazi, kwa safu ya wataalamu waliyo wengi, wanakinasibisha na utendaji. Hata hivyo, katika utafiti huu, hakikuchunguzwa kishazi katika sura hiyo. Isipokuwa tuliangalia jinsi ya mjengeko wa tungo kishazi, ulivyo katika kazi za wanafunzi hao.

Tuchunguze vifungu vifuatavyo:-

- i) ~ mtu yoyote yule anazungumza lahaja ya Kimakunduchi ~
- ii) ~ katika hasara ya siku ni~ siyoisahau ni hapa isemayo ~
- iii) ~ namalizia kusema ya kwamba ~
- iv) ~ Mwalimu nimpendae ni yule ambae ananipatia elimu hiyo inanipelekea kuwa karibu nae kila wakati ninapohitaji masomo yangu ili kuweza kuniongoza na kufikia rengo ninalohitaji ~
- v) ~ kuweza kunifuatia kunako *masomo yangu* na kuweza kunikosa *masomo yangu* pale ninapo kosea ~

Kuna vifungu vingi vya vishazi. Tumeviweka hivyo kama mifano. Katika kifungu na.i, tunabaini kosa la kiisimu katika neno ‘anazungumza’. Kwa mujibu wa kifungu hicho, neno hilo lilitakiwa libebe urejeshi, na hivyo kifungu hicho kisomeke hivi:

~ mtu yeyote yule anaazungumza lahaja ya Kimakunduchi ~

Bila ya kuweka urejeshi katika kifungu hicho, maana inayoweza kujitokeza haitakuwa sahihi. Maana, kinapochunguzwa kifungu hicho kama kilivyo, kinaashiria kwamba hakuna mtu asiyeweza kuzungumza lahaja ya Kimakunduchi. Jambo ambalo haliko sahihi. Kifungu cha pili, neno ‘hapa’ halistahiki kuwepo, na pia neno ‘ni~siyoisahau’ huwa ni neno moja, wala si maneno mawili kama lilivyoandikwa na baadhi ya wanafunzi hao. Aidha, kwa mujibu wa maelezo ya

kifungu hicho, hata neno ‘isemayo’ halihitajiki kuwepo. Maana, halina maana ya kisarufi (kwa hapo). Hivyo, kifungu hicho kilitakiwa kisomeke hivi:

~katika hasara za siku nisiyoisahau ni ~

Kifungu cha tatu, kina ziada ya neno ‘ya’ katika mtiririko wa Kiswahili sanifu hatusemi ‘namalizia kusema ya kwamba’ badala yake husema, ‘namalizia kusema kwamba’ au ‘namalizia kwa kusema kwamba’

Tunapokichunguza kifungu cha nne, tunabaini kuwa kuna makosa mengi ya kiisimu yamedhihiri. Kwanza, matumizi ya vituo, pili upatanishi wa kisarufi na tatu, kuna maneno ya kilahaja. Yaani kifungu chote hicho, tokea mwanzo hadi mwisho, hakina kituo chochote. Vituo ni muhimu sana katika tungo. Ndivyo vinavyomwezesha msomaji kupata uelewa ‘hasa’ wa kile kilichokusudiwa. Kutotumia vituo ni kuifanya tungo husika isieleweke ipasavyo. Aidha, utumizi wa maneno ya kilahaja katika sentensi za Kiswahili Sanifu hupoteza maana. Kwa mfano, neno ‘rengo’ ni lahaja ya Kimakunduchi, usahihi wake ni ‘lengo’.

4.5.1.2.3 Tungo Sentensi

Muundo wa tungo sentensi huzingatia mtiririko wa neno au kifungu cha maneno chenye kuleta maana iliyo kamili. Miundo ya sentensi ilitafitiwa na kupimwa katika kazi waliyopewa wanafunzi hao ya kuunda sentensi kwa mujibu wa maneno waliyopewa. Katika kipengele hiki, wanafunzi waliyo wengi walidhihirika kufanya vizuri. Hata hivyo, asilimia isiyopungua 25 ya wanafunzi hao iliharibu. Kwa mfano, walipotakiwa watunge sentensi kwa kutumia neno ‘kula’ na ‘cheza’ kwa kuzingatia njeo –na-, majibu ya baadhi yao yalikuwa hivi:

- i) Mimi nacheza ii) mimi nakula
 iii) mimi n'nacheza iv) mimi n'nakula

Hayo hayakuwa majibu sahihi ya kiisimu. Kuna mapungufu kadha. Miongoni mwa mapungufu hayo ni matumizi ya kiambishi cha nafsi ya kwanza (ni-) katika neno 'nacheza' na 'nakula'. Nafsi ni muhimu sana. Ndio inayotofautisha kati ya mtu wa kwanza umoja au wingi, mtu wa pili umoja au wingi, na mtu wa tatu umoja au wingi, na hivyo kumpa nafasi msomaji kumwelewa mtendaji wa tendo lililotajwa.

Pamoja na maelezo hayo, pia wanafunzi na walimu waliulizwa swali katika hojaji zao kuhusiana na athari za tungo. Swali lenyewe ni hili:

- iv) Tungo za Kiswahili Sanifu huathiriwa na lahaja ya Kimakunduchi kwa kiwango:
- a) Kikubwa sana (b) Kikubwa (c) Kati na kati
 d) Kidogo (e) Kidogo sana (f) Hakuna.

Majibu yalikuwa hivi:

i) Wanafunzi

- a) → 13.5% b) → 11.8% (c) → 13.5%
 d) → 15.2% e) → 32.2% (f) → 13.5%

ii) Majibu ya walimu

- a) → 0% b) → 33.3% (c) → 0%
 d) → 22.2% e) → 44.4% (f) → 0%

Majibu ya wanafunzi yanaweza kugawiwa katika makundi matatu. Kundi la 'A-C' lililopata asilimia 40, kundi 'D-E' lililo na asilimia 47, na kundi 'F' lilipata asilimia

13. Bila shaka, mwelekeo wa majibu hayo unatufahamisha kuwa zipo taathira za kilahaja katika tungo za Kiswahili Sanifu. Ingawa swali hili halikuainisha aina ya tungo husika, lakini uchambuzi uliofanyika hapo juu wa aina mbali mbali za tungo, umeshatosheleza kutuonyesha ni aina ipi ya tungo inayopata taathira zaidi. Ni dhahiri kuwa tungo vishazi huathirika zaidi kuliko aina zilizobaki. Asilimia 40 ya kiwango kilicho 'kikubwa sana' – 'kati na kati' ni asilimia kubwa na yenye kushitusha. Iwapo kila penye watoto mia, wanafunzi arubaini wameathirika na maneno ya kilahaja, ni dhahiri kuwa matumaini ya kufanya vizuri katika mitihani yao ya Taifa, ni madogo.

Kinachosikitisha zaidi, majibu ya walimu yamezidi kuumisha vichwa. Yaani, walimu wote wamekiri kuwepo kwa taathira hizo ndani ya maneno ya Kiswahili Sanifu. Kama hali ni hiyo, je somo la Kiswahili likoje katika mazingira hayo? Bila shaka usanifu wa somo hilo upo mashakani. Na katika mwelekeo huu, ni dhahiri kuwa natija inayopatikana ya somo hilo kwa wanafunzi hao, ni ndogo.

Awali tuliona katika matokeo ya wanafunzi hao ya mtihani wa Taifa 2010. Matokeo hayo yanaungwa mkono na matokeo ya mwaka 2008 ambapo jumla wanafunzi 81 walifanya mtihani wa Kiswahili. Kati ya hao, wanafunzi 35 hawakufaulu somo hilo, ilhali wanafunzi 46 ndiyo waliyofaulu kwa kiwango cha 'D' na 'C'. Kwa hakika asilimia 43 ya waliopata 'F' ni kubwa mno. Asilimia hiyo inaweza kuchukuliwa kama kigezo cha kuthibitisha dai letu kuhusu matumizi ya lahaja wakati wa somo la Kiswahili. Awali tumeona kuwa kuna baadhi ya masomo kama vile Dini ya Kiislamu, 'Civics', Kiarabu na hata Kiingereza, wanafunzi wameyafanya vizuri katika mtihani huo wa Taifa. Swali la kujiuliza, kwanini isiwe Kiswahili? Sababu

tunayo. Kwa mfano, somo la Kiingereza na Kiarabu, licha ya kuwa masomo hayo ni lugha, tena za kigeni, na licha ya kuwa kila lugha inazo kanuni zake, lakini wanafunzi wameyafaulu vizuri masomo hayo kwa vile hawakuwa na nafasi ya kuitumia lahaja yao ndani ya masomo yao. Wameshindwa kutokana na sababu mbili kubwa. Moja, lugha za masomo hayo ni tofauti, siyo kama ilivyo kwa Kiswahili na Kimakunduchi. Pili, kuna nadharia isemayo kuathiriana kwa lugha hutegemea na uasili wao. Yaani, lugha huathiriana iwapo zinatokana na asili moja. Hivyo, isingekuwa rahisi Kimakunduchi kuathiri Kiingereza au Kiarabu kwa vile hazina asili moja kama ilivyo kwenye lahaja sanifu na lahaja ya Kimakunduchi.

Aidha, haikuwa rahisi kwa matokeo ya Dini ya Kiislamu na yale ya 'Civics' kuathiriwa na lahaja hiyo kwa vile kinachozingatiwa wakati wa usahihishaji wa masomo hayo ni hoja zinazotolewa na wala si usahihi wa sarufi ya lugha husika (taz. Matokeo ya 2009).

4.5.2 Athari kwa Utoaji Elimu

Utafiti uizingatia kipengele hiki. Inaeleweka kuwa katika maisha ya kila siku, jamii hupata elimu juu ya mambo anuwai yahasuyo mazingira yao. Elimu ya afya, usafi, ndoa, uzazi, na ile yenye kutolewa shuleni kwa kila leo. Bila shaka, katika mawasiliano hayo, lugha inayotarajiwa kutumika ni lugha sanifu. Sababu kuu ya matumizi ya lahaja sanifu kwamba katika jamii yeyote lazima ndani yake, mna wakaazi wasiyo wenyeji wa eneo hilo. Ima wapo kwa sababu za kikazi, au wapo kwa mahamizi. Hivyo, ili jamii yote ifaidike, hulazimu kuitumia lugha sanifu kwa vile inaaminika kwamba inaunganisha wote. Aidha, hata taratibu za Serikali zinamtaka

mtoaji wa elimu hiyo atumie lugha sanifu badala ya lahaja yake. Hivyo, katika hojaji iliyotolewa kwa wanafunzi na kwa walimu, swali lifuatalo liliulizwa:

vi) Lahaja ya Kimakunduchi ina taathira katika utoaji wa elimu (kama elimu ya afya, usafi, n.k.) katika kiwango:

- | | | |
|-----------------|-----------------|------------------|
| a) Kikubwa sana | (b) Kikubwa | (c) Kati na kati |
| d) Kidogo | (e) Kidogo sana | (f) Hakuna. |

Wanafunzi 86 wa shule tatu zilizotafitiwa walilijibu, pamoja na walimu wote wa somo la Kiswahili katika shule hizo. Majibu yalikuwa na sura hii:

i) Majibu ya Wanafunzi

- | | | |
|------------|------------|-------------|
| a) → 8.1% | b) → 20.9% | (c) → 19.7% |
| d) → 17.4% | e) → 17.4% | (f) → 17.4% |

ii) Majibu ya Walimu

- | | | |
|------------|---------|-------------|
| b) → 11.1% | → b) 0% | → c) 33.3% |
| d) → 22.2% | e) → 0% | (f) → 33.3% |

Mtiririko wa majibu hayo unabainisha kuwa zipo athari za matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi katika utoaji wa elimu. Zipo sababu kadha za kusema hivyo, Kwanza, inahusiana na watafitiwa kwamba si watu wa kupanga. Ni wakaazi, wenyeji na wazaliwa wa eneo hilo. Ni dhahiri kuwa majibu waliyotoa, yana ukweli, tena ukweli mtupu. Pili, asilimia kubwa ya wanafunzi, na ya walimu imekiri kuwepo kwa athari hizo.

Tunaporejelea majibu hayo, wanafunzi waliokiri kuwepo kwa matumizi ya kiwango kilicho kati ya ‘kikubwa sana’ hadi ‘kati na kati’ 'A-C' ni asilimia 49, na wale waliyo katika kiwango cha ‘kidogo’ hadi ‘kidogo sana’ ni asilimia 34. Kwa pamoja viwango vyote hivyo ni vikubwa. Kwa mfano, asilimia 49 ni karibu ya nusu ya majibu ya watafitiwa wote. Kiutafiti, asilimia inayofikia kiwango hicho, huashiria kuwa jambo lililotafitiwa lipo kwa kiwango kikubwa. Tafsiri yake inadhihirisha kuwa wakati wa utoaji elimu katika sekta mbali mbali, matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi na yale ya lugha sanifu, huwa nusu kwa nusu.

Aidha, majibu ya walimu nayo yanaungana na wanafunzi wao, kwamba asilimia 44 iliyo kati ya kiwango ‘kikubwa sana’ hadi 'kati na kati' na asilimia 22 iliyo kati ya kiwango ‘kidogo sana’ ni dhihirisho kuwa zipo athari hizo katika utoaji wa elimu. Katika hali hiyo, sasa tuangalie jinsi athari hizo zinavyoathiri masomo yanayofundishwa.

4.5.2.1 Athari kwa Masomo Yanayofundishwa

Katika hojaji iliyotolewa kwa wanafunzi na kwa walimu, yalitakiwa mawazo kwa watafitiwa hao iwapo kuna athari kwa masomo yanayofundishwa. Swali lilikuwa hivi:

viii) Lahaja ya Kimakunduchi ina taathira katika masomo yanayofundishwa shuleni

katika kiwango:

- | | | |
|-----------------|-----------------|------------------|
| a) Kikubwa sana | (b) Kikubwa | (c) Kati na kati |
| d) Kidogo | (e) Kidogo sana | (f) Hakuna. |

Katika kutoa majibu ya swali hilo, wanafunzi 86 na walimu wote 9 walijibu katika sura ifuatayo:

i) Majibu ya Wanafunzi

a) → 15.2%	b) → 25.4%	(c) → 10.1%
d) → 18.6%	e) → 22.03%	(f) → 8.4%

ii) Majibu ya Walimu

b) → 0%	b) → 11.1%	(c) → 33.3%
d) → 44.4%	e) → 11.1%	(f) → 0%

Katika kuyachunguza majibu ya wanafunzi, tunabaini kuwa asilimia 91 ya wanafunzi wote imekiri kuwa zipo taathira za lahaja ya Kimakunduchi katika masomo yanayofundishwa. Asilimia 50 ipo katika kiwango kilicho kati ya kiwango 'kikubwa' na 'kati na kati'. Bila shaka asilimia hiyo inaonyesha jinsi ya kiwango cha taathira hizo kilivyo. Kiwango hicho kinatufunza kwamba katika masomo, lugha ya Kimakunduchi hupewa nafasi ya pekee. Tunaporejelea matokeo ya 2010, tunabaini kuwa kuna masomo kadha ambayo wanafunzi wamefeli sana. Kwa mfano, somo la 'civics' kati ya wanafunzi 165 ni wanafunzi 44 tu ndiyo waliyofaulu somo hilo ambao ni sawa na asilimia 27. waliobaki walifeli kwa kupata 'F'. Pia, kwa somo la Historia kati ya wanafunzi 117 waliyofanya mtihani huo, ni wanafunzi 34 tu ndiyo waliyofaulu ambao ni sawa na asilimia 29. Tunayazingatia masomo hayo kwa vile huingizwa katika masomo ya 'Arts' kama ilivyo kwa Kiswahili, Kiingereza, Kiarabu, na Dini ya Kiislamu. Yamkinika kwamba, wanafunzi walifeli katika kiwango hicho kikubwa kwakuwa wakati wanapojifunza darasani, lugha rasmi ya kufundishia masomo hayo huepukwa na badala yake hutumika zaidi lahaja ya Kimakunduchi.

Hili hupelekea kushindwa kuyaelewa nahata kuyajibu maswali ya mitihani hiyo kwa vile lugha ya mitihani waliyokabiliana nayo ni tofauti na ile waliyoitumia wakati wa kujifunza.

4.5.2.2 Athari katika Ujifunzaji

Swali jengine lililoulizwa kwa watafitiwa wa aina zote mbili, ni kuhusu athari za matumizi ya lahaja hiyo kwa ujifunzaji, swali lenyewe lilikuwa hivi:

ix) Lahaja ya Kimakunduchi huathiri utaratibu mzima wa ujifunzaji katika kiwango:

- | | | |
|-----------------|-----------------|------------------|
| a) Kikubwa sana | (b) Kikubwa | (c) Kati na kati |
| d) Kidogo | (e) Kidogo sana | (f) Hakuna. |

Wanafunzi 86 walilijibu swali hilo, pamoja na walimu wote wanaosomesha somo la Kiswahili katika shule zilizotafitiwa. Majibu yao yalikuwa hivi:

i) Majibu ya Wanafunzi

- | | | |
|-------------|-------------|--------------|
| b) —→ 20.9% | b) —→ 20.9% | (c) —→ 13.9% |
| d) —→ 19.7% | e) —→ 17.4% | (f) —→ 8.1% |

ii) Majibu ya Walimu

- | | | |
|-------------|-------------|--------------|
| a) —→ 0% | b) —→ 11.1% | (c) —→ 33.3% |
| d) —→ 44.4% | e) —→ 11.1% | (f) —→ 0% |

Majibu ya wanafunzi yanadhihirisha kuwepo kwa athari za matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi katika ujifunzaji. Asilimia 92 ya watafitiwa hao imelikiri jambo hilo. Ujifunzaji kwa matazamo wa kazi hii, umehusisha elimu tofauti kupitia masomo anuwai yanayofundishwa katika shule hizo. Hata hivyo, uzito wa ujifunzaji huo umo

ndani ya somo la Kiswahili. Asilimia hiyo ni kubwa na yenye kuashiria jambo moja la kimsingi. Kwamba lahaja ya Kimakunduchi hutumika wakati wa ujifunzaji. Hii inatoa mwelekeo kuwa wanafunzi wa Makunduchi hawawezi kujifunza kwa kutegemea lugha iliyo sanifu tu, lazima waweke mbele lahaja yao ndipo baadaye ifuate lugha sanifu. Iwapo tutayazingatia ipasavyo majibu hayo, wanafunzi waliyo kati ya kiwango kilichao ‘kikubwa sana’ na ‘kati na kati’ ni asilimia 56. Vyovyote iwavyo asilimia hii inamlazimisha kila msomi kuelewa uzito wa athari za lahaja hiyo katika ujifunzaji. Ingawa asilimia 8 imekana kuwepo kwa athari hizo, lakini mtazamo wa mtafiti anahisi kuwa kukana ukweli wenye kuungwa mkono na idadi kubwa ya watu hakuna uzito. Zipo sababu za kusema hivyo.

Tunasema kuwa ukanukaji wa baadhi ya wanafunzi hauna uzito kwa vile majibu yaliyotolewa na walimu wao, yamezama zaidi. Yamebainisha kwamba athari katika ujifunzaji, zipo tena, kwa asilimia 100. Tunaamini kuwa majibu haya ya walimu, licha ya kudhihirisha ukweli wa kuwepo kwa athari hizo, pia yamewageuka hata wanafunzi wao waliokataa kuwepo kwa athari hizo. Nini tunajifunza katika majibu ya watafitiwa wote? Kitu tunachokipata hapa kwamba ujifunzaji bila ya matumizi ya lahaja mama, hauwezi kufana. Kama ni hivyo, je matumizi hayo hayana madhara katika ujifunzaji huo? Bila shaka, madhara yapo, na ndiyo maana baadhi ya wanafunzi wanashindwa kujieleza kwa kutumia lugha sanifu pekee katika kazi zao mbali mbali kama insha, na hata katika kazi zao nyengine za kisarufi kama utungaji wa sentensi.

4.5.2.3 Athari katika Ufundishaji

Miongoni mwa mambo yaliyozingatiwa na utafiti huu ni swali zima la athari za lahaja ya Kimakunduchi katika ufundishaji. Wanafunzi na walimu waliulizwa swali lifuatalo:

x) Lahaja ya Kimakunduchi huathiri utaratibu wa ufundishaji kwa kiwango:

- | | | |
|-----------------|-----------------|------------------|
| a) Kikubwa sana | (b) Kikubwa | (c) Kati na kati |
| d) Kidogo | (e) Kidogo sana | (f) Hakuna. |

Wanafunzi 86 kati ya 90, walilijibu swali hilo. Aidha, walimu wote, 9 walijibu, na majibu yao yalikuwa hivi:

i) Majibu ya Wanafunzi

- | | | |
|------------|------------|-------------|
| a) → 11.7% | b) → 23.2% | (c) → 10.4% |
| d) → 33.7% | e) → 15.1% | (f) → 4.6% |

ii) Majibu ya Walimu

- | | | |
|------------|------------|-------------|
| a) → 0% | b) → 22.2% | (c) → 0% |
| d) → 33.3% | e) → 11.1% | (f) → 33.3% |

Mtiririko wa majibu ya wanafunzi unabainisha kuwa zipo athari za matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi wakati wa ufundishaji. Majibu hayo yanaonyesha kuwa asilimia 95 ya wanafunzi wote waliojibu imekiri kuwepo kwa athari hizo. Ufundishaji humuhusu zaidi mwalimu. Hivyo, mwanafunzi hubaki kama hakimu wa kuchunguza kitu gani anachokifanya mwalimu wake akiwa darasani. Wala haitarajiwi kwa mwanafunzi kuongea jambo lisilo ndilo dhidi ya mwalimu wake.

Mwanafunzi daima humuheshimu na kumthamini mwalimu. Huo ni utamaduni wa enzi na enzi na ndio urithi wa Watanzania na baadhi ya mataifa fulani ulimwenguni. Kwa uelewa huo ndipo tunapoweza kuyatathmini majibu ya wanafunzi hao kuwa ni sahihi. Kama hivyo ndivyo, yamkinika kuwa ufundishaji ni moja ya chanzo kinachowafanya wanafunzi wa Makunduchi kuathiriwa na matumizi ya lahaja yao. Haiwezekani kwa mwalimu kuitumia lahaja hiyo akiwa darasani, kisha, akamnasihi mwanafunzi asiitumiye. Waswahili husema, 'Mtoto hufuata kichogo cha mlezi wake.'

Nayo majibu ya walimu yanadhirishisha kuwepo kwa matumizi hayo wakati wa ufundishaji. Tumeona kuwa asilimia 66 imekubali kuwa yapo matumizi hayo wakati wa ufundishaji. Ingawa asilimia 33 imekataa, lakini mtafiti anahisi kuwa ukataaji wao hauna uzito. Kuna sababu kadha za kusema hivyo. Kwanza, majibu ya wanafunzi ambayo yamedhihirisha kuwepo kwa athari hizo kwa kiwango cha asilimia 95, Pili, walimu wenzao wamekiri hilo kwa asilimia 66. Tunavyoamini sisi, mwalimu mwenyewe hawezi kujisingizia wala kujikaribishia maovu. Bila shaka, wamekiri kwa kujiamini na kwa uhakika, na hivyo kumfanya mtafiti akubaliane na majibu hayo. Ushahidi wa hayo ni matokeo ya mtihani wa taifa wa wanafunzi wa shule ya Makunduchi kwa miaka mitatu tuliyoainisha hapo juu (2008, 2009 & 2010).

4.5.3 Taathira ya Athari Hizo

Pamoja na kuhoji athari mbali mbali za lahaja hiyo kwa somo la Kiswahili na kwa Kiswahili Sanifu, hatimae, mtafiti alitaka maoni kutoka kwa wanafunzi na kwa walimu yanayohusu taathira za athari hizo katika kipengele cha masomo, wanafunzi

na ufundishaji. Kilichobainika, wanafunzi waliyo wengi hawakutoa maoni yeyote, ilhali walimu wote waliongea juu ya taathira za athari hizo. Ni vyema tukachunguza maoni hayo. Tuanze na maoni ya wanafunzi, na swali lillikuwa hivi:

9. Kwa maoni yako, unadhani kuna taadhira gani ya athari hizo kwa:

a) Masomo

i)

ii)

iii)

b) Wanafunzi

i)

ii)

iii)

c) Ufundishaji

i)

ii)

iii)

i) Maoni ya Wanafunzi

a) Masomo

i) Iwapo mwanafunzi atafaulu na kutoka nje ya Makunduchi

ii) Kushindwa kujibu maswali ya mtihani wa Taifa kwa lugha sanifu

iii) Upungufu wa lugha iliyo sahihi, lugha ya kimji

iv) Wanafunzi hupata ufahamu mzuri wa masomo

Kwa ujumla hayo ndiyo maoni ya wanafunzi katika taathira za athari kwa masomo.

Maoni hayo yanaweza kuelezewa kwa ufupi kama hivi ifuatavyo:

Katika nukta ya kwanza, wanafunzi wamekusudia kutambulisha kwamba wakati wanapofaulu mitihani ya Taifa, na kisha kupangiwa shule zilizo kinyume na zile za maeneo yao, hupata usumbufu wa kutumia lugha fasaha, na hata ufahamuji katika masomo yao. Ndio maana, katika nukta ya nne wakakiri kuwa zama itumikapo lahaja ya Kimakunduchi, hupata ufahamu mzuri wa masomo.

Aidha, kwa upande mwingine wamekiri kuwa ipo taathira ya athari katika masomo. Nayo ni ile inayowapelekea kushindwa kuyajibu maswali ya mtihani wa Taifa wa somo la Kiswahili. Hivyo, kupelekea kupata natija hafifu. Nukta na.ii na na.iii, zote zinaongelea swali hili, ingawa katika nukta na. iii wameongezea kwa kusema ‘lugha ya kimji, wakiashiria lugha iliyo fasaha, ambayo kwao wao wameikusudia lugha sanifu.

b) Wanafunzi

- i) Hukitumia Kimakunduchi katika kujibu maswali
- ii) Hujisikia aibu wanapokutana na wenzao wanaoelewa Kiswahili Sanifu
- iii) Hushindwa kujiamini katika mazungumzo fasaha
- iv) Hufanya makosa ya kimaandishi wakati wa kujibu.

Katika kipengele hiki, maoni ya wanafunzi yameonyesha kuwa taathira zilizopo za athari hizo ni mbili kubwa. Kwanza, dosari ambazo hujitokeza wakati wa kujibu maswali ya mitihani yao, iwe ya shule au ya Taifa. Hili wamelithibitisha kupitia

nukta na,i na na.iv. Taathira hii ni mbaya. Hupelekea kuwakosesha alama bora katika somo lao la Kiswahili. Pili, dosari ya kimawasiliano, kwamba, pale wanapokutana na wenzao katika shule mbali mbali, mara nyingi hushindwa kujiamini katika kujieleza kwa hofu ya kufanya makosa ya kisarufi na hata kiufasaha wa lugha. Ndiyo maana, nukta na.ii na na.iii inaelekeza katika wazo hilo la udhaifu katika mawasiliano.

c) Ufundishaji

- i) Huliona somo la Kiswahili ni gumu hadi pale inapotumika lahaja yao.
- ii) Lahaja hiyo husaidia kwa vile maneno mengine ya Kiswahili Sanifu huwa hayaeleweki.

Kwa muhtasari nukta zote mbili zinaashiria kitu kimoja cha msingi. Kwamba, kwa wanafunzi wanahisi ipo haja ya kuitumia lahaja hiyo kwa vile huwasaidia katika uelewa wa somo husika. Wazo lao linapowekwa katika mizani, halionekani kuwa na dosari. Bali, kwa kuwa mtalaa wa somo umeshaongoza lugha sahihi ya kutumika darasani iwa ipi, ni dhahiri kuwa maoni ya wanafunzi hao, hayana msingi imara. Kinyume yake, iwapo watabaki na msimamo wa kuitumia lahaja yao katika kujibu mitihani, taathira kadha zitawakabili. Mojawapo ni kufeli kwa mtihani huo.

iii) Maoni ya Walimu

a) Masomo

- i) Kwa kutumia lahaja ufahamu wa masomo unakuwa mdogo
- ii) Hushindwa kujibu kwa Kiswahili Sanifu/fasaha
- iii) Masomo kudumaa kwa kutumia lahaja

- iv) Kushindwa kuandika kwa ufasaha wa lugha ya Kiswahili
- v) Kukosekana kwa mawasiliano ya Kiswahili fasaha
- vi) Inalazimu mwalimu atumie lahaja kwa kutoa mifano zaidi
- vii) Wakati mwengine wanapojibu mitihani yao ya Taifa kutumia lahaja zao
- viii) Baadhi ya wakati wanaingiza maneno ya Kimakunduchi katika kazi zao hasa somo la Kiswahili.

Katika kuyachunguza maoni ya walimu, yameonyesha taathira za kilahaja ambazo hupatikana kwa wanafunzi katika masomo yao. Walimu wanabainisha kwamba miongoni mwa taathira hizo kwa masomo ni kushindwa kujibu mitihani yao ya Taifa kiusanifu na kiufasaha. Aidha, inadhihirika kuwa hata ufaulu wa somo la Kiswahili unabaki mdogo kwa vile wanafunzi hao hutumia lahaja katika majibu yao.

Maoni hayo ya walimu ni muhimu na yenye kuhitaji uzingatifu uliyo mkubwa. Tunaamini kuwa walimu ndio watendaji wakuu wa shughuli za masomo. Kwani, ndio wenye kufundisha masomo hayo. Walimu kwa maumbile na hata tabia, ni wajuzi wa mambo mengi. Bila shaka, walichokiongelea ni sahihi kabisa. Zipo sababu za kusema hivyo.

Kwanza, walimu ndio wanaowafundisha wanafunzi hao, na hivyo wanawaelewa tabia zao zote. Wanamjua aliye hodari na asiye, anaesoma na asiye, na anaetumia lugha sanifu tu katika maandishi na asiyeitumia. Kwa hali hii, wanaujua udhaifu wa vijana wao katika matumizi ya lahaja kwa somo la Kiswahili. Pili, walimu ndio wanaowapa mazoezi ya darasani, mazoezi ya nyumbani, majaribio ya kila kipindi kifupi, na pia mitihani ya kila muhula. Hivyo, wanayajua majibu wanayoyatoa

pamoja na jinsi wanavyoitumia lahaja katika majibu yao. Tatu, baadhi ya walimu hao, yamkinika wamo wanaopata fursa ya kwenda katika usahihishaji wa mitihani ya Taifa. Kama hivyo ndivyo, bila shaka huzibaini karatasi za wanafunzi wao na jinsi zilivyo na makosa yenye kusababishwa na matumizi ya lahaja. Katika hali yoyote iwayo, maoni ya walimu yanatufanya tuamini kuwa zipo taathira za athari tulizoziorodhesha kabla kwa masomo. Ni dhahiri kuwa iwapo hakutakuwa na mabadiliko yoyote, wanafunzi hao wataendelea kuathirika dumu daima.

b) Wanafunzi

- i) Wanafunzi kushindwa kuzungumza Kiswahili Sanifu wakati anapoulizwa swali
- ii) Kupata matatizo makubwa wakati wa kujibu mitihani yao.
- iii) Kushindwa kutumia Kiswahili Sanifu katika maandishi yao
- iv) Kushindwa kujieleza kwa Kiswahili fasaha
- v) Kushindwa kutoa michango wakati wa majadala kwa Kiswahili Sanifu.

Kwa mujibu wa maoni hayo, yanaashiria kuwa bado walimu wanaendeleza wazo lao kwa wanafunzi. Kwamba, taathira za athari tulizoziainisha hapo kabla, humkabili zaidi mwanafunzi. Yaani, hushindwa kuukabili mtihani wao ipasavyo. Hawawezi kujibu kwa kutumia Kiswahili sanifu, na pia hushindwa hata kujieleza mbele ya wenzao. Hili lilishajiri katika insha zao. Tumbaini makosa kadha katika insha hizo, na miongoni mwake ni ufinyu wa kujieleza, dosari za utumizi a misamiati ya kilahaja, n.k. Hivyo, taathira hizo hatimae humpatia madhara mwanafunzi. Ambapo, badala ya kufanya vyema mtihani wake, hatimae hufeli na kupata daraja la chini katika cheti chake.

c) Ufundishaji

- i) Hauleti manufaa wala hauna mustakbali mzuri wa hapo baadae
- ii) Kwa baadhi ya wakati, malengo ya ufundishaji yanakosekana
- iii) Lahaja ikitumika sana hulemaza
- iv) Wakati wa ukaguzi, mwalimu hupata tabu kwa vile matumizi ya lahaja hayatakiwi. v) Bila ya lahaja wanafunzi hawaelewi na bila ya kuelewa, hulala darasani.

Maoni ya walimu katika muktadha wa taathira za athari za ufundishaji yapo kudhihirisha mwelekeo ule ule wa kuanguka wanafunzi katika masomo yao. Neno ‘mustakbali’ liliomo katika nukta ya kwanza linaashiria mwelekeo wa mitihani, na kwamba kwa matumizi ya lahaja wakati wa ufundishaji, huwafanya wanafunzi wapate ulemavu katika matumizi ya lahaja yao.

Aidha, maoni yameonyesha pia iwapo matumizi ya lahaja yatakithiri katika ufundishaji, kwanza malengo ya somo lenyewe hupotea. Pia na hata wanapokuja wakaguzi, mwalimu husika hupata tabu ya kulisomesha somo kwa vile anashindwa kujidhibiti katika kuacha kuitumia lahaja hiyo. Madhara ya kuwa katika hali hiyo. Kwanza kubaki na hofu, pili kushindwa kuliwasilisha somo ipasavyo, na hatimae kuwapelekea wanafunzi wakose uelewa. Jambo hili mwishowe iwapo litakuja swali la mtihani ndani ya mada hiyo, mwanafunzi atashindwa kulijibu.

4.6 Hitimisho

Sura hii imefanya uwasilishaji na uchambuzi wa data ili kukamilisha malengo ya utafiti wetu. Hili limefanikiwa pale ambapo sifa mbalimbali za lahaja ya

Kimakunduchi zimetolewa na baadaye athari mbalimbali za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu nazo zikabainishwa. Uchambuzi huu unadhihirisha kwamba, kuitenga lugha na jamii yake ni jambo gumu lisilowezekana kabisa. Tunayasema haya kwa sababu wanafunzi pamoja na walimu katika shule teule za Makunduchi husisitizwa kuwasiliana kwa kutumia Kiswahili Sanifu wakati wote wawapo katika mazingira ya shule. Pamoja na msisitizo huo bado Kimakunduchi nacho kinatumika na hivyo kukiathiri Kiswahili sanifu. Maelezo zaidi kuhusiana na suala hili yanatolewa katika sura inayofuata hapa chini.

SURA YA TANO

5.0 MATOKEO YA UTAFITI

5.1 Utangulizi

Mwisho wa kazi ya utafiti, ni budi yadhahirike matokeo ya kazi hiyo. Katika utafiti huu kuna matokeo kadha yaliyobainika. Ni vyema tukayaorodhesha pamoja na ufafanuzi wake.

5.2 Matokeo

Itakumbukwa kwamba awali, katika sura ya kwanza, kazi hii ilitanguliza maswali ya utafiti ambayo kwa kiasi fulani yamesaidia katika kuiongoza kazi hii hadi kumalizika kwake. Aidha, wakati tunayazingatia matokeo ya utafiti huu tumelazimika mara nyingi kuyarejelea na kuyahusisha na maswali ya utafiti yaliyomo kwenye sura ya kwanza (ang. 1.4). Hivyo, matokeo haya ni majibu ya maswali hayo.

5.2.1 Matokeo Kutokana na Maswali ya Utafiti

Swali Na. 1 liliuliza, ‘Je ni zipi sifa za kiisimu za lahaja ya Kimakunduchi? Dhihiriko la majibu ya swali hili limo katika vipengele anuwai vya kazi hii. Utafiti umezibaini sifa hizo, na hivyo, kuashiria kuwa lahaja ya Kimakunduchi inazo sifa zake za kiisimu kama ilivyo katika lugha nyenginezo zilizo sanifu na hata zisizo. Miongoni mwa sifa zilizobainika.

Moja, utafiti umebaini kuwa lahaja hiyo inazo nafsi zenye idadi sawa na nafsi za Kiswahili sanifu. Ingawa baadhi ya viambishi vinavyowakilisha nafsi hizo ni tofauti kiumbo na viambishi vya Kiswahili Sanifu. Utofauti huo unajitokeza katika nafsi ya pili (umoja na wingi) na katika nafsi ya tatu (umoja). Wakati Kiswahili Sanifu

kinatumia kiambishi ‘u’ cha nafsi ya pili umoja na *m-/mu-* katika wingi, Kimakunduchi hutumia kiambishi ‘ku’- katika umoja na ‘wa’ – katika wingi. Ilhali, kiambishi kiambata cha nafsi ya tatu (umoja) ya Kiswahili Sanifu ni ‘a-’, Kimakunduchi huwakilishwa na kiambishi ‘ka-’.

Pili, utafiti umeabaini kuwa Kimakunduchi kina njeo zake ambazo huzitumia katika kubainisha wakati muafaka wa tendo litarajiwalo kufanyika. Maumbo ya njeo za Kimakunduchi hayatofautiani na yale ya Kiswahili Sanifu isipokuwa kwa njeo ya wakati wa baadaye. Kiswahili Sanifu hutumia ‘-ta-’ kama ni kiambishi njeo kinachowakilisha wakati ujao. Ilhali, Kimakunduchi huwakilishwa kwa njeo ‘-cha-’. Kwa mfano, ‘kachakuja kesho’ ni sentensi sahihi ya Kimakunduchi yenye tafsiri sawa na ‘*Atakuja kesho*’ katika Kiswahili Sanifu.

Hivyo, ‘ka’ ni kiambishi nafsi ya tatu, ‘-cha-’ ni kiambishi cha njeo ya wakati ujao, ‘--kuj-’ mzizi wa neno, na ‘-a’ ni kiambishi cha mnyambuliko.

Sifa nyengine ya kiisimu iliyobainika, kwamba Kimakunduchi kinayo sifa ya umilikishi. Wakati Kiswahili Sanifu umilikishi wake hujitokeza (zaidi) katika maneno mawili yaliyo mbalimbali kama ‘kaka yangu’ na ‘rafiki yako’, katika Kimakunduchi, umilikishi wake hudhihirika ndani ya neno moja. Yaani, aghalabu nomino husika huambatanishwa na kiambishi kimilikishi na kulifanya neno hilo libebe umilikaji ndani yake. Kwa mfano, ‘rafikiyo’ badala ya ‘*rafiki yako*’ na ‘mtotowe’ badala ya ‘*mtoto wake*’. Hivyo, kiambishi ‘-yo’ cha ‘rafikiyo’ na ‘-we’ cha ‘mtotowe’, ndivyo vinavyobeba dhima ya umilikishiji.

Nne, utafiti umebaini kuwa lahaja ya kimakunduchi inayo tabia (sifa) ya kudondosha viambishi katika maneno. Udondoshaji huo unaweza kujotokeza kwenye majina (nomino), vitenzi na baadhi ya aina nyenginezo za maneno kama vivumishi na viwakilishi. Kwa mfano:

Nda - *Nakwenda* (kitenzi)

Chi - *Chini* (kielezi)

Chi - *Nchi* (Nomino)

Hiyo ni baadhi tu ya mifano ya udondoshaji katika Kimakunduchi. Kwa mifano zaidi rejelea uchambuzi wa data katika sura ya nne.

Swali Na.2 liliuliza, ‘Lahaja ya Kimakunduchi ina athari gani katika msamiati wa Kiswahili Sanifu? Kwa ujumla swali hili lilitafitiwa kwa kina. Ikabainika kuwa lahaja ya Kimakunduchi inatumika katika kiwango kikubwa katika darasa, kupelekea athari mbalimbali kwa msamiati wa lugha ya Kiswahili Sanifu. Miongoni mwa athari zilizodhihirika ni kama hivi ifuatavyo:

Moja, utafiti umebaini kuwa msamiati wa Kiswahili Sanifu huathiriwa mno na lahaja ya Kimakunduchi, na hivyo kupelekea baadhi ya wanafunzi hao kushindwa kutumia maneno sanifu katika maongezi na kwenye kazi zao za darasani. Jambo hilo hutilia shaka kwamba, hata katika mitihani yao ya Taifa, huegemea katika dosari hiyo. Wakati wanafunzi hao walipotakiwa watunge sentensi, majibu yao yalionesha athari za lahaja hiyo katika misamiati ya Kiswahili Sanifu. Ipo mifano mingi kama vile neno ‘*ninanakula*’ kuandikwa ‘*nakula*’ au ‘*ninacheza*’ kuwa ‘*nacheza*’.

Pili, utafiti umebainisha kuwa kwa baadhi ya wakati, umbo lenyewe la neno hubeba ulahaja. Kwa mfano, neno ‘*ninakula*’ huandakwa kilahaja ‘n’*nakula*’ au neno ‘*ninacheza*’ huandikwa ‘n’*nacheza*’. Katika mtiririko huo huo, ndipo inapojitokeza kuona kuwa hata tungo zao hubainika kutungwa katika hali ya ulahaja. Ipo mifano kadha iliyoainishwa katika sura ya nne hapo juu ikishadidia hoja hii.

Swali na.3 liliuliza, ‘Je ni zipi taathira za athari hizo kwenye matumizi ya Kiswahili Sanifu katika maeneo yaliyo rasmi? Kupitia mwongozo wa swali hilo, utafiti ulizibaini taathira anuwai ambazo zimetokana na athari mbalimbali za Kimakunduchi kwa Kiswahili Sanifu. Tuzingatia haya yafuatayo:

- Taathira katika masomo. Hapa kuna taathira za namna mbili. Moja, wanafunzi kutoelewa vyema masomo yao hadi pale lahaja ya Kimakunduchi itumike. Wazo hili linatupa imani kuwa lahaja yao inawasaidia katika ufahamu wao, na hivyo katika kufaulu kwao. Pili, kwa utumizi wa lahaja hiyo, ingawa inawasaidia katika ufahamu wao, wanashindwa kuitumia lahaja sanifu ipasavyo, na hivyo kupelekea kukosa natija nzuri katika somo lao la Kiswahili.

Taathira nyengine iliyobainishwa katika kazi hii, inahusika na ujifunzaji. Yaani, tendo zima la kujifunza huathiriwa na matumizi ya lahaja hiyo. Hivyo, maongezi ya wanafunzi katika darasa, na katika mijadala yao haiwezi kufana bila ya matumizi ya lahaja hiyo. Kwa utaratibu huu ndipo wanafunzi wanaposhindwa kulielewa somo lao la Kiswahili vile inavyotakiwa. Kwa mfano, mazoea yao ya kuitumia lahaja huwafanya wasahau baadhi ya kanuni za Kiswahili Sanifu za misamiati, sauti na miundo ya sentensi zenyewe.

Taathira ya tatu iliyobainika, inahusu ufundishaji. Kama inavyoeleweka, ufundishaji humuhusu mwalimu. Naye ni kigezo kwa kila analolisema na analolifanya kwa wanafunzi wake. Bila shaka, iwapo mwalimu ataitumia lahaja hiyo katika ufundishaji wake, wanafunzi kwa upande wao watakithiri katika kuitumia. Jambo hilo hatimae huwafanya wanafunzi hao walemae, wa waitumie lahaja yao si katika maongezi pekee, na hata katika maandishi yao. Hatimaye, ndipo wanaposhindwa kujibu maswali ya mitihani ya darasani, na yamkinika mitihani ya Taifa.

Mbali ya taathira hizo, utafiti umebaini kuwepo kwa taathira nyengine kama vile:

- Kushindwa kuitumia lugha sanifu katika shughuli za kitaaluma na katika hadhara za watu ambao ni wazoefu wa Kiswahili Sanifu.
- Wanafunzi kujisikia aibu pale wanapotoka nje ya Makunduchi. Hivyo, yamkinika hata kuongea hushindwa kwa kujisikia 'haya'.

5.2.2 Taathira za Dhana za Kinadharia

Tunaporejea kiunzi cha nadharia ya utafiti huu, tuliainisha nadharia iliyotumika kuongoza utafiti huu. Nadharia yenyewe ilikuwa ni 'Nadharia ya Umaumbo' ambayo iliasisiwa na Mikhailovick Baklitin (1917) wa Urusi.

Katika nadharia hiyo, mambo matatu makubwa yameongelewa ambayo yalikubaliana na mwelekeo wa utafiti huu. Mambo yenyewe yalihusu lugha kama mseto wa vijilugha mbalimbali, lugha na makundi ya watu katika jamii, na tatu lugha na mivutano ya mifumo mbalimbali.

a) Lughu kama Mseto wa Vijilugha Mbalimbali

Kiswahili ni lugha yenye hadhi nyingi, zenye kuongozwa na hadhi mbili kubwa. Yaani, hadhi ya Taifa na nyingine ni hadhi ya lugha rasmi. Bila shaka, urasmi wake umeibuka baada ya kusanifiwa kwake, ilhali kubaki kama lugha ya Taifa imetokana na kuteuliwa kwake kisiasa.

Kiswahili licha ya hadhi hizo, inakubalika kwa asili yake ni mchanganyiko wa vijilugha mbalimbali (lugha mseto). Tunaelewa kuwa Kiswahili Sanifu kimetokana na lahaja ya Kiunguja Mjini, lakini Kiswahili chenyewe ni mchanganyiko wa lahaja mbalimbali za Kiswahili. Ndiyo maana lahaja hizo zinaitwa ‘Lahaja za Kiswahili’ kuashiria kuwa ni vijilugha vilivyotokana au vilivyoizaa lugha hiyo.

Kama lahaja hizo zinakubalika kuwa ndio zenye kuijenga lugha hii ya Kiswahili, ni dhahiri kuwa athari za lahaja hizo zitajitokeza ndani ya lugha mama. Kwa bahati njema, wakati tunaitafiti mada hii, tulibaini kuwa kuna taathira kadha za Kimakunduchi ndani ya lugha sanifu. Kwa mfano, tunayo mazoea ya kulitumia neno “mwanawe” au “mwanangu” kama msamiati ulio rasmi. Bali tunaporejea data tuliyoichambua katika sura ya nne ya utafiti huu tunaona kuwa mtindo wa umilikishi wa kuunganishwa katika nomino moja umo ndani ya lahaja ya Kimakunduchi. Hivyo, si kosa hata kidogo kusema kuwa lahaja hii nayo imeiathiri lahaja ya Kiswahili Sanifu.

Aidha kwa mwelekeo huohuo, ndipo inapoadifu wanafunzi na hata walimu kuitumia lahaja yao wakati wa somo la Kiswahili, kwamba, wakiadini kuwa lahaja yao ni mojawapo ya vijenzi vya Kiswahili.

b) Lugha na Makundi ya Watu katika Jamii

Awali wakati tunajadili nadharia ya umaumbo ilitudhihirikia kuwa mtafiti alipaswa ateue makundi maalumu ya watu wa kuwatafiti. Ni dhahiri kuwa kundi aliloteua lina sifa maalumu, sifa ya usomi. Wasomi kwa hulka yao, ni waelewa na watambuzi wa mambo. Ni wafafanuzi na wenye sababu za ufafanuzi wao. Wasomi wana lugha yao ambayo ni tofauti na lugha za makundi mengineyo. Lugha hii ya wasomi huwa na kanuni zake ambazo haikubaliki kuziepuka, hususani iwapo lugha hiyo itatumika katika mazingira maalumu kama yale ya shuleni au darasani

Msomi anaekiuka miiko ya lugha ya darasani hutafsirika amevunja sheria, na mwenye kuvunja sheria, huadhibiwa. Ni jambo linaloeleweka kuwa uvunjaji wa sheria unaweza kujitokeza kwa maamuzi ya ‘makusudi’ yaani kwa ‘kujua’ au kwa ‘kutojua’. Ingawa hivyo, adhabu za uvunjaji sheria hazizingatii kwa kuchunguza iwapo mkosaji alikuwa anajua au hajui kuwa ‘anavunja sheria’

Katika utafiti huu tulibaini kuwa upo uvunjaji wa sheria za lugha hiyo ya darasani. Uvunjaji huo hufanyika katika hali zote mbili – Ima hali ya makusudi, kama tulivyoona baadhi ya maoni ya watafitiwa. kwamba, bila ya matumizi ya lahaja hiyo, hawawezi kufahamu somo husika. Au wakati mwingine sheria kuvunjwa bila kutojua. Kwa vyovyote vile utumizi wa lahaja darasani, hususani wakati wa somo la Kiswahili ni ukiukaji wa sheria. ingawa, kwa baadhi ya wakati utumizi huo huwa ni wa ‘ulazima! Kwanini? Kwa sababu iwapo wanafunzi wanakiri kuwa ili walielewe somo, lazima wafahamishwe kwa kilahaja, ni budi itumike. Ingawa hivyo, mazoea ya kuitumia katika ufahamisahaji na ufahamishwaji, hatimae wanafunzi huitumia

kimaandishi. Matokeo ya kuitumia lahaja katika maandishi, ndipo wanafunzi wanapoanguka katika kutafuta alama zao.

Kwa ujumla, hivyo ndivyo nadharia hiyo ilivyotumika kwa kutuongoza katika kupata majibu muafaka ya utafiti huu. Sura inayofuata inatoa hitimisho, muhtasari pamoja na mapendekezo ya utafiti wote.

SURA YA SITA

6.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

6.1 Utangulizi

Sura hii imeongelea mambo matano muhimu. Yaani, imeonyesha muhtasari wa utafiti wote. Katika nukta hii mtafiti ametaja baadhi ya mambo muhimu yaliyomo katika kila sura. Kipengele kilichojadiliwa ni matokeo muhimu ya utafiti. Hapa, kumedhihirishwa matokeo mbalimbali yaliyobainika wakati wa utafsiriji wa data, na hata wakati ambao mtafiti alipitia maandishi mbalimbali ya lahaja ya Kimakunduchi. Kitu kingine, utafiti umejaribu kubainisha taathira za dhana za kinadharia zilizotumika ndani ya kazi hii. Mwisho, utafiti umemalizia kwa kuonyesha mapendekezo mbalimbali ambayo mtafiti anaamini kuwa lau yatafanyiwa kazi yamkinika yanaweza kuleta tija hapo baadae.

6.2 Muhtasari na Hitimisho la Utafiti

Utafiti huu umejengeka kwa sura tano ambazo ndani yake muna mambo muhimu yaliyojadiliwa. Sura ya kwanza yenye anuani 'Utangulizi' imekusanya na kufafanua usuli wa mada ambao umebainisha chanzo cha kuibuka mada hiyo na kupelekea kufanyiwa utafiti. Pia, imeongelea juu ya mada ya utafiti ambapo kuna hoja zilizojadiliwa kuhusu nukta hiyo. Aidha, sura imegusia kwa kutaja lengo kuu pamoja na malengo mahsusi ya utafiti huu. Mwisho, imemalizia kwa kuonyesha maswali ya utafiti, upeo wa utafiti, umuhimu wa utafiti pamoja na kubainisha marejeleo ya vitabu.

Sura ya pili yenye anuani 'Sifa za Kiisimu za Kimakunduchi', kwa jumla, imejaribu kubainisha baadhi ya sifa za lahaja hiyo katika maeneo kadha. Kwa mfano, katika

sauti za Kimakunduchi, katika maumbo ya maneno, maneno ya Kimakunduchi na viambishi vya nafsi, maumbo ya maneno na njeo, maumbo ya maneno na umilikishi, maumbo ya maneno na udondoshaji, maumbo ya maneno na utofauti wa msamiati, na maumbo ya maneno na ukanushi. Aidha, sura imezingatia swali la mjengeko wa tungo za Kimakunduchi katika hali ya kiima na kiarifu, hali ya ujitoshelezaji na katika hali ya upatanishi wa kisarufi.

Katika sura ya tatu, utafiti umeongelea juu ya matumizi ya lugha ya darasani ambapo mtafiti ameichunguza lugha hiyo jinsi ilivyo. Je, ni sanifu, ni ya kilahaja, au ni mchanganyiko wa usanifu na lahaja. Bila ya shaka, tumeona kuwa lugha ya darasani ni mchanganyiko. Tumbaini kuwa mchanganyiko huo upo kwa wanafunzi na walimu. Aidha, sura imeonyesha kuwa usanifu wa lugha hiyo umo katika maandishi ya matini ya walimu na katika lugha ya muhtasari wa masomo, pamoja na kutaja sababu zenye kupelekea usanifu huo kupatikana katika maeneo hayo pekee. Mwisho, sura ikamalizia kwa kuonyesha lugha ya kazi za wanafunzi ikoje.

Sura ya nne, yenye anuani 'Athari za Kimakunduchi kwa Kiswahili Sanifu', ndani yake kuna athari mbalimbali zilizoongelewa. Kwa mfano, mtafiti amezichunguza athari za kiisimu kwenye sauti, kwenye maneno na kwenye tungo. Pia, aliangazia juu ya athari hizo kwa utoaji wa elimu katika kipengele cha masomo yanayofundishwa, katika ujifunzaji na katika ufundishaji. Mwisho, sura imemaliza kwa kutaja na kufafanua taathira za athari hizo kwa masomo, kwa wanafunzi na kwa ufundishaji. Kwa ujumla, sura hii ndiyo iliyokuwa sura mama katika utafiti huu ambayo ilizifasiri data zilizokusanywa. Athari anuwai zilibainika kama zilivyoorodheshwa katika sura ya nne.

Sura ya tano imekamilisha mtiririko mzima wa kazi hii. Hapa mtafiti ameeleza kwa ufupi juu ya muhtasari wa utafiti, matokeo muhimu, taathira za dhana za kinadharia, na mwishowe, kutaja mapendekezo ya utafiti wenyewe.

6.3 Mapendekezo ya utafiti

Baada ya kumaliza zoezi zima la utafiti huu, kuna mapendekezo kadha yamejitokeza ambayo mtafiti anaamini kuwa iwapo yatafanyiwa kazi, yatasaidia katika maendelao ya jamii.

Moja, kuna umuhimu wa kuzitafiti lahaja mbalimbali kwa nia ya kuweka kumbukumbu ya vizazi vya baadaye. Ni dhahiri kuwa kadiri jamii inavyobadilika, ndivyo na lahaja zao zinavyobadilika. Turejee mfano wa maelezo ya Mh. Rais wa nne wa Zanzibar, wakati akitoa dibaji yake katika kamusi ya Msamiati wa Pekee wa Kikae, amesema kuwa ndani ya kamusi hiyo mna baadhi ya misamiati ambayo hata yeye binafsi hana kumbukumbu nayo. Naye, Chum (1994) alisisitiza kwa kusema 'kamusi ya lahaja ya kikae imetengenezwa kwa madhumini maalumu... pamoja na maingiliano ya jamii nyinginezo utakuta kuwa ndimi za vizazi vilivyotangulia zinahitilafiana sana na ndimi za vizazi vya siku hizi seuze hivyo vijavyo...! (uk. 1-2). Bila shaka, mwenye macho haambiwi tazama. Kauli ya Chum inatilia mkazo wazo la kutafitiwa lahaja zote kwa lengo la kumbukumbu.

Pili, lazima ibuniwe njia mbadala katika ufundishaji wa wanafunzi darasani, ambapo matumizi ya lahaja yataepukwa. Lengo si kuichukia au kuidharau lahaja hiyo, bali kutekeleza sera inayohimiza matumizi ya lugha rasmi katika maeneo yaliyo rasmi. Kushindwa kutekeleza sera hiyo ni kuhatarisha maisha ya wanafunzi ya kitaaluma.

Kwa ajili hiyo ili kuwajengea mazingira mazuri watoto wetu, tutumie njia mbadala katika kuwafunza vijana hao. Bila shaka, mbinu mbadala hizo zinaweza kutafitiwa kwa kupitia makundi mbalimbali ya watu.

Tatu, Lahaja ya Kimakunduchi ina maeneo mengi ya kuitafiti. Mojawapo linatokana na ile kauli ya Mh. Rais Idris Abdul Wakil isemayo "... ni shida sana kwa mtu ambaye hakuzaliwa na hasa kukulia Makunduchi kuweza kukisema kwa ufasaha mzuri. Watu wengi hujaribu kukisema lakini mara hushindwa katika matamshi. Kwa sababu hiyo, baadhi ya watu hufikiri kuwa Kikae ni lugha tofauti na Kiswahili. Hivyo tamko la kusema kuwa baadhi ya watu wanahisi kwamba Kikae (Kimakunduchi) ni tofauti na Kiswahili, ni tamko linalohitaji kufanyiwa kazi. Na hivyo, watafiti walitafiti tamko hilo ili kujua iwapo Kimakunduchi ni lahaja ya Kiswahili au la. Tena tusichelewe maana kadiri ya siku zinavyoongezeka, yamkinika mabadiliko makubwa yakatokea ndani ya lahaja hiyo.

MAREJELEO

Babbie, E., (1999), *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Chum, H. (1994) *Msamiati wa Pekee wa Kikae*. Sweden. Nordic Association Of African Studies.

Chiraghdin na Mnyampala, M. (1977) *Historia ya Kiswahili*. Dar es Salaam. Oxford University Press.

Khamis, A. (2008) “Jadi na Utamaduni wa Mswahili wa Zanzibar” *katika Utamaduni wa Mzanzibari*. Zanzibar. Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA).

Kitala, (2006), *Mapitio ya ripoti ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania*. Dar es Salaam: Haijachapishwa.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A. (2006), *Proposal and Thesis Writing: Introduction*, Nairobi, Paulines Publications Africa.

Kothari, R. C. (1990), *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Delhi, New Age International (P) Limited

Kothari, C.R., (2008), *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Maganga, C. (1997) *Historia ya Kiswahili*. Dar es Salaam Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

- Masebo, J. na Nyagwine, N. (2006) *Jitayarishe kwa Kiswahili kidato cha 3 na 4*
Dar es Salaam. The General bodi Sellers ltd.
- Masebo, J. na Nyangwine, A. (2007) *Nadharia ya Lugha Kiswahili 1 Kidato cha 5
&6*, Dar es Salaam. Nyambari Nyangwine Publishers.
- Masebo, J. na Nyangwine, N. (2008) *Kiswahili Kidato cha 3 na 4*. Dar es Salaam,
Nyambari Nyangwine Publishers.
- Massamba, D na wenzake (2001) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA),
Sekondari na Vyo*, Dar es Salaam, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
(TUKI).
- Mbaabu, I. (1991) *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Nairobi Longman Kenya
Ltd.
- Mbaabu, I. (2003), "Sheng English Dictionary: Diciphering East Africa Underworld
Language", Dar es Salaam: TUKI.
- Mhilu, G. na Masebo, J. (2008) *Kiswahili kwa Shule za Sekondari Kidato cha Tatu*.
Dar es Salaam. Nyambani Nyangwine Publishers.
- Mochiwa, Z.M (1979), 'The Impact of Kiswahili Language on ethnic Languages. A
case Study from Handeni District', Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa),
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mohamed, S. (1984) "Urban Versus Rural Swahili (A Study of Pemba Varieties)",
Zanzibar. (Haijachapishwa).

- Muhura, C. (2009) *Kiswahili - Lugha na Fasihi Kidato cha 3*, Dar es Salaam. Kiiya Publishers.
- Msanjila, Y.P. (2006), “Nadharia katika Isimu Jamii: Mjadala Unaoendelea”, katika *Mulika* na. 27, TUKI: Dar es Salaam, kur. 40-48.
- Mwansoko, H.J.M (2008) ‘‘Nafasi ya Lahaja katika Kuendeleza Msamiati na Istilahi za Kiswahili Sanifu’’ katika Kiango, J.G (mh.) *Ukuzaji wa Isilahi za Kiswahili*, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Rubanza, Y.I (1979), 'The relationship between Kiswahili and other African Languages. The case of Kihaya', Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Stigand, C. (1915) ‘‘A Study of the Morphology of Standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu and Kimakunduchi’’, Zanzibar: Haijachapwa.
- Wamitila, K. (2002) *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi. Phoenix Publishers Ltd.
- Whiteley, W. (1956) *Ki-mtang'ata (A Dialect of the Mrima Coast – Tanganyika)*. Kampala. East African Swahili Committee.

KIAMBATANISHO I

Maswali ya mtafiti kwa mwalimu wa Somo la Kiswahili

1. Jina

2. Umri Kazi

3. Jinsia Makaazi

4. Anwani yako: Sanduku la Posta

.....

5. Simu

6. Kwa mawazo yako ni nini lahaja?

.....

7. Naomba unitajie sauti zilizomo katika jedwali lifuatalo kwa lahaja ya Kimakunduchi. Kisha, kwa kila sauti, ambatanisha mfano wa neno moja lililotumia sauti hiyo.

Sauti ya Kiswahili Sanifu	Sauti ya Lahaja ya Kimakunduchi	Mfano kutoka kitenzi (ikiwa unao)	Mfano kutoka Nomino (ikiwa unao)	Mfano kutoka kihusishi (ikiwa unao)
/a/ - angalia				
/b/ - baba				
/ - chachift/				
/d/ - dada				
/e/ - embe				
/f/ - fagia				
/g/ - gogo				
/h/ - haramu				
/i/ - inda				
/ - Jumamosij/				
/k/ - kazi				

9. Naomba katika kila njeo ya hizi zifuatazo, nitungie sentensi mbili kwa lahaja ya Kimakunduchi, na kisha niwekee tafsiri yake kwa Kiswahili Sanifu

NJEO	LAHAJA YA KIMAKUNDUCHI	KISWAHILI SANIFU
Njeo ya wakati wa sasa (-na-)		
i. Kula	1.	1.
ii. Cheza	2.	2.
Njeo ya wakati uliopita (muda mfupi: -me-)		
i. Imba	1.	1.
ii. Soma	2.	2.
Njeo ya wakati uliopita (muda mrefu: -li-)		
i. Uza	1.	1.
ii. Nunua	2.	2.
Njeo ya wakati ujao (-ta-)		
i. Sema	1.	1.
ii. Sikiliza	2.	2.
Njeo ya mazoea (-hu-)		
i. Lima	1.	1.
ii. Vuna	2.	2.

10. Katika kila kifungu ya vifuatavyo, chagua jawabu lililo sahihi na kisha, weka alama ya 'vema' (√) ndani ya mabano yaliyo mbele yake

i) Wakati wa Somo la Kiswahili, matumizi ya Lahaja ya Kimakunduchi huwa:

- a) Makubwa sana ()
 b) Makubwa ()
 c) Kati na kati ()
 d) Madogo ()
 e) Madogo sana ()
 f) Hakuna ()

ii) Wanafunzi huitumia lahaja ya Kimakunduchi wakati wa Somo la Kiswahili katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()

- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

iii) Walimu huitumia lahaja ya kimakunduchi wakati wa Somo la Kiswahili katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

iv) Kiswahili Sanifu huathiriwa na sauti za lahaja ya Kimakunduchi katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

v) Maneno ya Kiswahili Sanifu huathiriwa na lahaja ya Kimakunduchi katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

vi) Tungo za Kiswahili Sanifu huathiriwa na lahaja ya Kimakunduchi kwa kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

vii) Lahaja ya Kimakunduchi ina taathira katika utoaji wa elimu (kama elimu ya afya, usafi, n.k.) katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

viii) Lahaja ya Kimakunduchi ina taathira katika masomo yanayofundishwa shuleni katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

ix) Lahaja ya Kimakunduchi huathiri utaratibu mzima wa ujifunzaji katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

x) Lahaja ya Kimakunduchi huathiri utaratibu wa ufundishaji kwa kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

11. Kwa maoni yako, unadhani kuna taathira gani ya athari hizo kwa:

- a) Masomo
 - i).....
 -
 - ii).....
 -
 - iii).....
 -
- b) Wanafunzi
 - i).....
 -
 - ii).....
 -
 - iii).....
 -
- c) Ufundishaji
 - i).....
 -
 - ii).....
 -
 - iii).....
 -

ASANTE KWA MSAADAWAKO

KIAMBATANISHO II

Maswali ya mtafiti kwa wanafunzi wa Sekondari wa Skuli za Makunduchi

1. Jina
2. Umri Kazi
3. Jinsia Makaazi
4. Anwani yako: Sanduku la Posta

5. Simu

.....

6. Kwa mawazo yako ni nini lahaja?

.....

.....

.....

.....

7. Naomba katika kila njeo ya hizi zifuatazo, nitungie sentensi mbili kwa lahaja ya Kimakunduchi, na kisha niwekee tafsiri yake kwa Kiswahili Sanifu

NJEO	LAHAJA YA KIMAKUNDUCHI	KISWAHILI SANIFU
Njeo ya wakati wa sasa (-na-)		
i. Kula	1.	1.
ii. Cheza	2.	2.
Njeo ya wakati uliopita (muda mfupi: -me-)		
i. Imba	1.	1.
ii. Soma	2.	2.
Njeo ya wakati uliopita (muda mrefu: -li-)		
i. Uza	1.	1.
ii. Nunua	2.	2.
Njeo ya wakati ujao (-ta-)		
i. Sema	1.	1.
ii. Sikiliza	2.	2.
Njeo ya mazoea (-hu-)		
i. Lima	1.	1.
ii. Vuna	2.	2.

--	-------	-------

8. Katika kila kifungu cha vifuatavyo, chagua jawabu lililo sahihi na kisha, weka alama ya 'vema' (✓) ndani ya mabano yaliyo mbele yake

i) Wakati wa Somo la Kiswahili, matumizi ya Lahaja ya Kimakunduchi huwa:

- a) Makubwa sana ()
- b) Makubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Madogo ()
- e) Madogo sana ()
- f) Hakuna ()

ii) Wanafunzi huitumia lahaja ya Kimakunduchi wakati wa Somo la Kiswahili katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

iii) Walimu huitumia lahaja ya kimakunduchi wakati wa Somo la Kiswahili katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

iv) Kiswahili Sanifu huathiriwa na sauti za lahaja ya Kimakunduchi katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

v) Maneno ya Kiswahili Sanifu huathiriwa na lahaja ya Kimakunduchi katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

vi) Tungo za Kiswahili Sanifu huathiriwa na lahaja ya Kimakunduchi kwa kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

vii) Lahaja ya Kimakunduchi ina taathira katika utoaji wa elimu (kama elimu ya afya, usafi, n.k.) katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

viii) Lahaja ya Kimakunduchi ina taathira katika masomo yanayofundishwa shuleni katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

ix) Lahaja ya Kimakunduchi huathiri utaratibu mzima wa ujifunzaji katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
-) c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

x) Lahaja ya Kimakunduchi huathiri utaratibu wa ufundishaji kwa kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()

- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

xi) Lahaja ya Kimakunduchi huathiri wanafunzi kwa kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

xii) Lahaja ya Kimakunduchi huathiri walimu katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

9. Kwa maoni yako, unadhani kuna taathira gani ya athari hizo kwa:

a) Masomo

i).....
.....

ii).....
.....

iii).....
.....

b) Wanafunzi

i).....
.....

ii).....
.....

iii).....
.....

c) Ufundishaji

i).....
.....

ii).....

iii).....

KIAMBATANISHO III

Maswali ya mtafiti kwa wanafunzi wa Msingi na Kati wa Skuli za Makunduchi

1. Jina

2. Umri Kazi

3. Jinsia Makaazi

4. Anwani yako: Sanduku la Posta

5. Simu

6. Katika kila kifungu cha vifuatavyo, chagua jawabu lililo sahihi na kisha, weka alama ya 'vema' (✓) ndani ya mabano yaliyo mbele yake

i) Wakati wa Somo la Kiswahili, matumizi ya Lahaja ya Kimakunduchi huwa:

a) Makubwa sana ()

b) Makubwa ()

c) Kati na kati ()

d) Madogo ()

e) Madogo sana ()

f) Hakuna ()

ii) Wanafunzi huitumia lahaja ya Kimakunduchi wakati wa Somo la Kiswahili katika kiwango:

a) Kikubwa sana ()

b) Kikubwa ()

c) Kati na kati ()

d) Kidogo ()

e) Kidogo sana ()

f) Hakuna ()

iii) Walimu huitumia lahaja ya kimakunduchi wakati wa Somo la Kiswahili katika kiwango:

a) Kikubwa sana ()

b) Kikubwa ()

c) Kati kati ()

d) Kidogo ()

e) Kidogo sana ()

f) Hakuna ()

iv) Kiswahili Sanifu huathiriwa na sauti za lahaja ya Kimakunduchi katika kiwango:

a) Kikubwa sana ()

b) Kikubwa ()

c) Kati na kati ()

d) Kidogo ()

- e) Kidogo sana ()
 f) Hakuna ()

v) Maneno ya Kimakunduchi hutumika katika Somo la Kiswahili katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
 b) Kikubwa ()
 c) Kati na kati ()
 d) Kidogo ()
 e) Kidogo sana ()
 f) Hakuna ()

vii) Maneno ya Kimakunduchi hutumiwa katika utoaji wa elimu (kama elimu ya afya, usafi, n.k.) katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
 b) Kikubwa ()
 c) Kati na kati ()
 d) Kidogo ()
 e) Kidogo sana ()
 f) Hakuna ()

viii) Maneno ya Kimakunduchi hutumiwa katika masomo yanayofundishwa shuleni katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
 b) Kikubwa ()
 c) Kati na kati ()
 d) Kidogo ()
 e) Kidogo sana ()
 f) Hakuna ()

ix) Wanafunzi wanapojifunza hutumia maneno ya Kimakunduchi katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()
 b) Kikubwa ()
 c) Kati na kati ()
 d) Kidogo ()
 e) Kidogo sana ()
 f) Hakuna ()

x) Walimu wanapofundisha hutumia maneno ya Kimakunduchi katika kiwango:

- a) Kikubwa sana ()

- b) Kikubwa ()
- c) Kati na kati ()
- d) Kidogo ()
- e) Kidogo sana ()
- f) Hakuna ()

7. Kwa mawazo yako, unadhani kuna matatizo yoyote ya kuyatumia maneno ya

Kimakunduchi katika:

a) Masomo

i).....
.....

ii).....
.....

iii).....
.....

b) Wanafunzi

i).....
.....

ii).....
.....

iii).....
.....

c) Ufundishaji

i).....
.....

ii).....
.....

iii).....
.....

ASANTE KWA MSAADAWAKO

KIAMBATANISHO V

Kuhusu matini ya mwalimu wa Somo la Kiswahili

1. Jina
2. Darasa unalofundisha
3. Naomba unipatie matini yako yeyote uliyoiandaa kwa ajiili ya wanafunzi wako wa Somo la Kiswahili

ASANTE SANA KWA MSAADA WAKO